**Tanzania** yaokoa trilioni 1.5/- uwekezaji wa DP World bandarini

UKURASA 2



**Hatima** kesi ya Kabendera, Vodacom leo

UKURASA 7



**WHO** kusaidia nchi wanachama kukabili Mpox

UKURASA 19

Jumatano Agosti 21, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581775

The Guardian digital

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




GUNDOGAN ATANGAZA RASMI KUSTAAFU SOKA

UKURASA 22

# Sakata 'binti wa Yombo' lafukuta

• **TLS**, Zitto wajitosa na hoja nyeti; kesi mpya yafunguliwa dhidi ya 'afande'...

*Endelea Ukurasa 3*

"Aliyeagiza yale yote yafanyike yuko wapi? Kwani sheria zetu ni za watu fulani na wengine haziwagusi? Afande akamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria"



Rebeca Gyumi

"Binti huyo kukaa mikononi mwa Jeshi la Polisi si salama; ahifadhiwe na taasisi za haki za binadamu"



Zitto Kabwe

"TLS inapongeza hatua za kufikishwa mahakamani wanaodaiwa kutenda uhalifu huo, lakini tunataka aliyesababisha kufanyika kitendo hicho afikishwe mahakamani mara moja"



Boniface Mwabukusi

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**PROF. JANABI: INACHUKUA MIAKA 10 - 15 KUTAMBUA UNA KISUKARI**




Rais Samia Suluhu Hassan akikagua moja ya madarasa baada ya kufungua Skuli ya Maandalizi Dk. Samia Suluhu Hassan, Kusini Unguja, jana, iliyojengwa kwa hisani ya Benki ya NMB. Wengine ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohammed Mussa (wa pili kulia) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Ruth Zaipuna (kushoto). **PICHA: IKULU**

## Kizimbani kwa shtaka kuingilia mfumo wa matokeo UDSM, IFM

UKURASA 5

TAMASHA LA KIZIMKAZI

## NMB yamkabidhi Samia skuli ya milioni 800/-

UKURASA 5

**MICHEZO** ATEBA KAMILI SIMBA SC KUIVAA FOUNTAIN GATE UK.24

**MAONI,** UK.6

# Majaliwa ataka madereva kutunza siri za mabosi wao

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameelekeza madereva wa serikali wanapokuwa na viongozi katika magari, wajitahidi kutunza siri kwa kuwa wanabeba dhamana ya nyaraka za serikali.

Pia amewataka kutokuingilia na kuchangia maongezi wakati viongozi wakizungumza na watu wengine kwa njia ya simu, hasa wanapokuwa ndani ya gari.

Waziri Mkuu aliagiza hayo jana jijini Arusha wakati akifungua Kongamano la Tatu la Madereva wa Serikali.

“Unakuta kiongozi anazungumza kwa simu akiwa ndani ya gari kisha dereva anaingilia mazungumzo pasipo kujua kiongozi huyo anazungumza na nani, huo ni utovu wa nidhamu, ukosefu wa maadili, uvunjivu wa nidhamu na ni kinyume cha sheria na kanuni za udereva,” alisema Waziri Mkuu.

Majaliwa alisema madereva wa serikali wanapaswa kuwa na siri pindi wanapokuwa na viongozi katika magari kwa kuwa wanabeba nyaraka za serikali na suala la siri ni muhimu kwa kuwa siri ni sehemu ya nyaraka hizo.

Waziri Mkuu pia aliagiza taasisi na mashirika ya umma kutoa rukhsa madereva kuhudhuria mikutano yao ya kitaaluma na kuwalipa stahiki zao zote.

Kuhusu hoja ya michango ya madereva hao kuchelewa kupelekwa kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Majaliwa alisema serikali ilishaelekeza makato yote kwa madereva yafanyike moja kwa moja Hazina.

Vilevile, aliigiza Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kufanya msawazo kwa watumishi ili isitoke mtumishi yupo na ameajiriwa, lakini hana kazi ya kufanya.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya, alisema chama hicho ni cha hiari na kilianzishwa mwaka 2013.

Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Serikali Tanzania, Flora Mnyandavile, alisema katika kongamano hilo, madereva 1,300 wamehudhuria mkutano huo. Kati yao, 1,200 wanatoka Tanzania Bara na 140 wanatokea Tanzania Zanzibar.

Alisema chama hicho kina wanachama zaidi ya 7,241. Kati yao, wanaume ni 7,191 na wanawake ni 50.

# Tanzania yaokoa trilioni 1.5/- uwekezaji wa bandarini

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usimamizi Bandari Tanzania (TPA) imesema kupungua kwa tozo ya ziada ya usafirishaji meli tangu meli kufika na muda wa kuhudumiwa kupungua kutoka siku 30 (Novemba na Desemba mwaka jana) hadi siku 10, kumewezesha Tanzania kuokoa Dola milioni 600 (Sh. trilioni 1.5).

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa, alisema meli za makasha zinatumia siku tatu hadi nne kushusha mzigo kwenye gati, hali iliyochangia kampuni za meli kupunguza tozo hiyo ambayo ni Dola 1,000 kwa kasha.

Mbosa alisema TPA inahudumia wastani wa makontena milioni 1.2 kwa mwaka na kwamba kutokana na kampuni ya MSC kupunguza tozo, imesukuma kampuni zingine za meli kupunguza.

Alisema mabadiliko makubwa ikiwamo kupunguza tozo yaliyofanyika bandarini, meli za kampuni hiyo zitakuja moja kwa moja Bandari ya Dar es Salaam tofauti na mwanzo, walikwenda Bandari ya Mombasa.

“Kama tunahudumia milioni 1.2 kwa mwaka, nusu ni kontena 600,000, maana yake tuna uwezekano wa kuokoa Dola milioni 600, hizo gharama zimeshuka. Fedha hizi zililipwa na Watanzania, hivyo watapata unafuu kwa sababu gharama imepungua. Haya ni mafanikio ya Rais Samia Suluhu Hassan,” alisema.

Awali Ofisa Mtendaji Mkuu wa DP World Tanzania na Mashariki ya Kati, Martin Jacob, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa, uwekezaji kwenye Bandari ya Dar es Salaam umeanza kuonesha matunda baada ya serikali kuokoa Dola za Marekani milioni 600 (Sh. trilioni 1.5) katika miezi minne tangu kuanza kwa mkataba wake na kampuni ya DP World.

Alisema ndani ya miezi minne, maboresho yaliyofanyika yamesababisha kupungua gharama za usafirishaji mizigo na kumechochea ukuaji wa uchumi, kuongeza ajira kwa wananchi na kuiweka Tanzania katika nafasi ya kuwa lango kuu la kiuchumi Afrika Mashariki.

Jacob alisema mafanikio hayo yanaimarisha nafasi ya Tanzania kama kitovu cha biashara Afrika Mashariki na Kati na yanaonesha uthabiti wa Rais Samia Samia Suluhu Hassan katika kusimamia rasilimali za taifa kwa manufaa ya Watanzania.

Alitaja mafanikio kuwa ni pamoja na kupungua kwa muda wa meli kusubiri; meli za mizigo ya kontena sasa zinaweza kutia nanga na kupakua shehena mara tu zinapowasili na kuboresha muda wa mzunguko na kupunguza gharama kwa kiasi kikubwa.

Alisema ubia wa kimkakati na ushirikiano na DP World umesababisha Shirika la Meli la Mediterrenean (MSC) kuondoa gharama ya ziada ya Dola 1,000 kwa kila kontena, ikiokoa Tanzania takriban Dola milioni 600 kila mwaka.

Alisema kuwa katika uzalishaji, uendeshaji kreni umeboreshwa, na uzalishaji umekuwa ukiongezeka kwa kasi kutoka Mei hadi Julai 2024, na bandari hiyo kufanikiwa kushughulikia meli zake kubwa.


**MTIBWA SUGAR ESTATES LTD**

**TAARIFA KWA UMMA**

Kufuatia mabadiliko madogo ya sheria ya sukari ya mwaka 2024 na kanuni zake. Kiwanda cha sukari cha Mtibwa kinapenda kuutaarifu umma kwamba sukari ya Mtibwa Sugar inapatikana katika maduka yafuatayo:

| S/No | CustomerName | Area/Region | Contacts |
|---|---|---|---|
| 1 | BrysonMwanga | Bagamoyo | 0715309439 |
| 2 | MaimunaKilala | Bagamoyo | 0659095699 |
| 3 | MasamiGeneralTradersLtd | Bagamoyo | 0768912028 |
| 4 | Al-NaeemEnterprisesLtd | DaresSalaam | 0754784131 |
| 5 | HambaHauleCo.Ltd | DaresSalaam | 0715850439 |
| 6 | TanzaniaCashSales | DaresSalaam | 0716848484 |
| 7 | YusuphJumaSempombe | DaresSalaam | 0715098485 |
| 8 | DonatiLombuli | Dodoma | 0715431517 |
| 9 | H.M.Gulamali | Dodoma | 0715043707 |
| 10 | JafariRajabuGuka | Dodoma | 0788089061 |
| 11 | JeradKamnyongoKagosi | Dodoma | 0767883932 |
| 12 | ChitembeleEnterprisesLtd | Gairo-Morogoro | 0756366806 |
| 13 | AllyHemedAlly | Handeni-Tanga | 0676949659 |
| 14 | FatumaKhalidShafii | Handeni-Tanga | 0624294472 |
| 15 | DoradoInvestment | Kariakoo-DaresSalaam | 0715083666 |
| 16 | MartinKasambala | Kariakoo-DaresSalaam | 0714643181 |
| 17 | MatemaBeachEstateLtd | Kariakoo-DaresSalaam | 0757555999 |
| 18 | JasminMwidadiJuma | Kibaha | 0754847227 |
| 19 | ValerianLyanzile | Kilosa | 0676453767 |
| 20 | KorogweGeneralTrading-Company | Korogwe | 0620804109 |
| 21 | SelemanMohamedJuma | Mkindo-Madizini | 0715542005 |
| 22 | PatrickKajegeChagunya | Mlandizi | 0713992366 |
| 23 | Felister | Morogoro | 0677050629 |
| 24 | JamesMsteriMdesa | Morogoro | 0755195385 |
| 25 | LigambaGeneralLtd | Morogoro | 0715560600 |
| 26 | MohamedIdha | Morogoro | 0783200000 |
| 27 | MolisaTradingCo.Ltd | Morogoro | 0715229361 |
| 28 | MpendaOneLtd | Morogoro | 0715308732 |
| 29 | ThabitandSons | Morogoro | 0715384343 |
| 30 | ThabitMohamedIslam | Morogoro | 0715081122 |
| 31 | Tulashashewinome Ltd | Mvomero-Morogoro | 0757597125 |
| 32 | ManenoLubehoMweshemi | Mwanza | 0753085649 |
| 33 | MotoMathiasIfulu | Shinyanga | 0785911917 |
| 34 | NassoroSalumAbdallah | Shinyanga-Kishapu | 0685169667 |
| 35 | YSMInternational | Songea | 0765999786 |
| 36 | JimmyProsperMarco | Tabora | 0763168477 |
| 37 | LeonardKasoniManaha | Tabora | 0620808060 |
| 38 | MolaKasomiLupembe | Tabora | 0768637551 |
| 39 | SaidMohamedSarahani | Tabora | 0784440435 |
| 40 | ZakariaGahise | Tabora | 0786625600 |
| 41 | A.A.ShehozaandCompanyLtd | Tanga | 0672179791 |
| 42 | AbusheheHussenQuffi | Tanga | 0787265434 |
| 43 | AmriNassoroSaid | Tanga | 0713465994 |
| 44 | FatumaKajuna | Tanga | 0715954900 |
| 45 | FatumaKassimSidy | Tanga | 0715222090 |
| 46 | JumaAbdallahKhery | Tanga | 0784492257 |
| 47 | DaudiMasona | Turiani-Madizini | 0788205638 |
| 48 | ElikanaMathiasMahungija | Turiani-Madizini | 0673088830 |
| 49 | KushanaMakenzi | Turiani-Madizini | 0710555983 |
| 50 | MabulaMakenzi | Turiani-Madizini | 0759445035 |
| 51 | ShabaniAbelMihurumbo | Turiani-Madizini | 0716928579 |
| 52 | UshetuGeneralLtd | Turiani-Madizini | 0628503246 |
| 53 | MbuyaofUrambo | Urambo | 0715235555 |

Pia kwa yeyote atakaye hitaji sukari toka kiwandani awasiliane nasi kwa namba zifuatazo:

**0677 049 226 / 0714 990 633**

**Utawala: Mtibwa Sugar Estates Ltd**



**KAGERA SUGAR LIMITED**

**TAARIFA KWA UMMA**

Kufuatia mabadiliko madogo ya sheria ya sukari ya mwaka 2024 na kanuni zake. Kiwanda cha sukari cha Kagera kinapenda kuutaarifu umma kwamba sukari ya Kagera Sugar inapatikana katika maduka yafuatayo:

| S/No | Customer Name | Region | Contact |
|---|---|---|---|
| 1 | Kyosk Digital Services Limited | Arusha/Mwanza | 0717298789 |
| 2 | Mr.Ngusa Mashauri Kazi | Bariadi-Shinyanga | 0767272553 |
| 3 | Mr Modestus Alex Ruhinda | Biharamuro-Kagera | 0765354366 / 0675580688 |
| 4 | Amir Hamza (T) Ltd | Bukoba-Town | 0762494714 / 0683889488 |
| 5 | Kabula Charles Kilasa | Chato-Geita | 0765038714 / 0755286338 |
| 6 | Megamack Enterprises (T) Limited | Geita-Town | 0784364755 |
| 7 | George R Clemence | Kagongwa-Kahama | 0786460633 / 0769123603 |
| 8 | Bernard Kalamu Lyaka | Kahama-Town | 0653563123 / 0612050723 |
| 9 | Bwana Ni Mwema Company Limited | Kahama-Town | 0622470238 / 0784493042 |
| 10 | Ngunda Maduhu Kubagwa | Kahma-Shinyanga | 0685222223 |
| 11 | Impression 99 Limited | Kakonko-Kigoma | 0784291037/0754391037 |
| 12 | Kadudusi John Mbunabune | Kakonko-Kigoma | 0755413118 |
| 13 | Mr.Sokoine Enosi Makasi | Kaliua-Tabora | 0786049946 |
| 14 | Salehe Mohamed Salehe | Kaliuwa-Tabora | 0784897869/0767799004 |
| 15 | Longino Kamugisha Wilbard | Karagwe-Kagera | 0757260066/0787732770 |
| 16 | Alfred Joseph Kiloloma | Kasulu-Kigoma | 0762111678/0757223215 |
| 17 | Ahmadi Ramadhani | Kasulu-Kigoma | 0756825163/0748192435 |
| 18 | Zacharia Charles Ndabahaliye | Kasulu-Kigoma | 0757729961/0613729961 |
| 19 | Nyandwi Company Limited | Kibondo-Kigoma | 0758000723/0687506990 |
| 20 | Peter Deogratias Nyamaliza | Kibondo-Kigoma | 0765432878 |
| 21 | Kivumu Investment Group Limited | Kigoma-Town | 0784157242/0754754315 |
| 22 | A.M.Jaffer Supplies Limited | Kigoma-Town | 0784786750/0679867320 |
| 23 | Mariam Abdul Kisura | Kyerwa/Bukoba-Kagera | 0742968285/0622561966 |
| 24 | Amri Issa Bikaria | Kyerwa-Kagera | 0782305534/0765050941 |
| 25 | Murishid Hassan Miyonga | Kyerwa-Kagera | 0743603850 |
| 26 | Rulinda Enterprises | Missenyi-Kagera | 0784742050/0767071757 |
| 27 | Kobra Enock Petro | Mpanda-Katavi | 0759061835/0784747893 |
| 28 | Mashala Gilas Lyogo | Mpanda-Katavi | 0763105000/0766933076 |
| 29 | Jeremiah Kajeki Mwenda | Mpanda-Katavi | 0766384354/0788925165 |
| 30 | Shayakye Trading Co Limited | Muleba-Kagera | 0752456990/0764560507 |
| 31 | Johansen Company Limited | Muleba-Kagera | 0744291745 |
| 32 | Jifs Co & General Supplies | Ngara-Kagera | 0767223819/0784223819 |
| 33 | Rafael Aron Mtaka | Rwamugasa-Geita | 0755332435 |
| 34 | Leonard Kasoni Manaha | Shinyanga-Town | 0620808060/0784387515 |
| 35 | Gilitu Enterprises Limited | Shinyanga-Town | 0754222999/0752085034 |
| 36 | Thabit And Sons Limited | Tabora-Town | 0767384343/0754384343 |
| 37 | Zakaria Japhet Gahise | Tabora-Town | 0753154350 |
| 38 | V H Shah & Co. | Mwanza | 0786428728 |

Pia kwa yeyote atakaye hitaji sukari toka kiwandani awasiliane nasi kwa namba zifuatazo:

**0784 410 576 / 0767 410 576**

**Utawala: Kagera Sugar Limited**

## Wazee watoa kilio kutoheshimiwa mabasi mwendokasi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZEE wanaotumia usafiri wa umma jijini Dar es Salaam, wamelalamika ukosefu wa maadili unaofanywa na vijana kwa kutoheshimu sheria za kuwapisha kuketi kwenye viti.

Malalamiko hayo wameyatoa hasa kwenye usafiri wa mabasi yaendayo kwa haraka, maarufu mwendokasi ambayo yametengewa vitu maalum kwa wazee na wenye ulemavu.

Wakitoa malalamiko hayo, wazee wa Wilaya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, walidai kuwa wanafunzi na vijana hawawapishi kwenye viti vilivyotengwa kwa ajili yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali la Good Samaritan Social Services Tanzania, Elisha Mwamkinga, alimwambia Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hassan Bomboko, kuwa wazee wakiwa ndani ya mabasi hayo wanalazimika kusimama wakati viti vilivyotengwa kwa ajili yao vinakaliwa na wanafunzi au vijana wenye nguvu.

"Serikali imetuletea mabasi ambayo ndani yake kuna viti vilivyotengwa kwa ajili ya wazee na watu wenye ulemavu, lakini viti hivyo tunakuta vimekaliwa na vijana wenye nguvu ambao hujifanya wanachat na simu zao, huku wanafunzi wakijifanya wamesinzia kwenye viti hivyo wakituacha sisi wazee tumeshikilia mabomba," alilalamika.

Mkutano huo uliandaliwa na mashirika yasiyo ya kiserikali Wilaya ya Ubungo (Nacongo) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

Mkuu wa wilaya akijibu hoja hiyo, alisema huo ni mmomonyoko wa maadili na alisihi familia kuangalia suala la malezi kwa watoto kuanzia utotoni.

"Wazazi ndio kioo cha jamii, ikiwa watakuwa na tabia za ajabu, moja kwa moja watoto watarithi tabia hizo hivyo kuwa na taifa lisilokuwa na maadili, ni wajibu wa mzazi kumfunza mtoto maadili mema, heshima kwa wakubwa na kumchagulia marafiki wa kucheza nao, pamoja na kumsimamia kushika na kufuata misingi ya dini yake," alisema.

Aliongeza kuwa watoto wengi siku hizi wanalelewa na mabibi zao, mama akiwa anashughulishwa na dunia au wafanyakazi wa majumbani ambao wengi wao nao ni watoto.



Madiwani wa Kata za Manispaa ya Kinondoni, wakipiga kura wakati wa kikao cha kumchagua Naibu Meya wa Manispaa hiyo na kupitisha taarifa ya utendaji ya mwaka 2023/2024, Dar es Salaam jana, ambapo Diwani wa Kata ya Kunduchi, Michael Urio aliibuka mshindi wa nafasi hiyo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Sakata la 'Binti wa Yombo' lafukuta

**Jenifer Gilla na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Mawakili Tanganyika (TLS) kimelitaka Jeshi la Polisi kumfikisha mahakamani mtu anayetajwa 'afande', anayedaiwa kutuma vijana wanne kumbaka na kumlawiti binti anayedaiwa mkazi wa Yombo Dovya, wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam, kisha video ya ukatili huo kusambazwa mitandaoni.

Pia kimetoa wito kwa Jeshi la Polisi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuimarisha madawati ya jinsia katika majeshi, ikiwamo kuweka watumishi wenye weledi wa kukabiliana na matukio ya ukatili wa kijinsia ipasavyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Dar es Salaam, Rais wa TLS, Boniface Mwabukusi alisema chama kinapongeza hatua za kufikishwa mahakamani wanaodaiwa kutenda uhalifu huo, lakini wanataka aliyesababisha kufanyika kitendo hicho afikishwe mahakamani mara moja.

Alisema chama hicho kimedhamiria kumweka wakili atakayefuatilia maendeleo ya shauri la kesi hiyo, ili kuhakikisha haki ya binti huyo inapatikana na waliohusika wanachukuliwa sheria.

Wakili Mwabukusi pia alipongeza hatua zilizochukuliwa na Jeshi la Polisi kumwajibisha Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Theopista Mallya kutokana na kauli yake iliyotafsiriwa kama kupuuzia madhila makubwa aliyoyapata binti huyo.

"TLS itaona namna bora ya kuweka wakili atakayekuwa akifuatilia ili kuona maendeleo ya shauri lile, yatakavyokuwa yakiendelea na kuhakikisha kuwa haki za binti yule hazipotei," alisema Wakili Mwabukusi.

Alisema chama hicho kinatoa wito kwa Jeshi la Polisi na wizara yenye dhamana kuimarisha madawati ya jinsia kwa kuweka watu wenye uwezo na wanaochukizwa na vitendo hivyo ili kuyashughulikia kwa weledi.

Katika ukurasa wake wa X, Wakali Peter Madeleka, aliandika: "Leo (jana) tarehe 20 Agosti 2024, Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma imesajili malalamiko namba 000058901 ya Paul Emmanuel Kilasa Kisabo dhidi ya ...(anataja jina anayedaiwa ofisa wa jeshi) anayedaiwa kutuma vijana wambake na kumlawiti binti wa Yombo."

Malalamiko hayo yanasema kuwa 'afande' (jina halipo) katika tarehe isiyojulikana Mei mwaka huu eneo la Swaswa, Jiji la Dodoma alitenda kosa la kuwezesha ubakaji kwa kundi (akataja majina ya washtakiwa wanne wanaodaiwa kubaka na kulawiti) dhidi ya binti huyo, jambo ambalo ni kinyume na utu.

Mbunge wa zamani wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe alisema binti huyo kukaa mikononi mwa Jeshi la Polisi si salama na akapendekeza ahifadhiwe na taasisi za haki za binadamu.

"Inatakiwa taasisi za haki za binadamu zimchukue huyu binti kisheria kutoka polisi. Tanpol siyo mahala salama kwa binti huyu," alidai Zitto.

"Badala ya kupata msaada huko, atakuwa ameteseka sana kisaikolojia. THRDC nini kinawashinda kumchukua binti chini ya uangalizi wenu?

"Kumwacha huyu binti Polisi kwa siku moja zaidi ni kumtesa sana, hao Polisi wataanza kumshambulia kuwa amemfukuzisha mwenzao," alidai.

Kauli hiyo ya Zitto inafanana na ile iliyotolewa na Shirika la Msichana Initiative pamoja na mashirika yanayotetea haki za wanawake Dar es Salaam, ambao wametaka binti huyo apate msaada wa kuhifadhiwa na taasisi tofauti na Jeshi la Polisi ili haki ionekane inatendeka.

Mkurugenzi wa Shirika la Msichana Initiative, Rebeca Gyumi, alisema ni vyema anayedaiwa kuagiza vijana waliotekeleza kitendo hicho akakamatwa.

"Aliyeagiza yale yote yafanyike, yuko wapi? Kwani sheria zetu ni za watu fulani na wengine haziwagusi? 'End impunity', afande akamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria," alisema Rebeca.

**WALIOPOTEA**

Katika hatua nyingine, Wakili Mwabukusi amesema Baraza la Uongozi la TLS imeazimia kuwafungulia mashtaka kwa majina yao wale wote wanaotajwa kuhusika kwenye kadhia ya kukamata, kuteka na kutesa kiholela wananchi na imeandaa timu ya mawakili kwa ajili kufanya kazi hiyo.

Alilitaka Jeshi la Polisi kuwaeleza Watanzania kuwa uchunguzi wao kuhusu watu hao umefikia wapi na kuwa wanalifuatilia jambo hilo kwa karibu na hatua sizipochukuliwa hawatosita kufanya hivyo.

"Ni wito wetu kwa mamlaka, kutoa orodha ya wananchi wasiojulikana walipo, hawa ni Watanzania, uhai ni kitu cha thamani kuzidi kitu kingine chochote. Tunalitaka Jeshi la Polisi kutoka mbele za umma na kuwaeleza wamefikia wapi, uchunguzi kuhusu watu hao umefikia wapi," alisema.

Wakili Mwabukusi alisema TLS pia inatoa wito kwa serikali kuchukua hatua za haraka kurejesha huduma za kijamii kwa wananchi wa Ngorongoro, ikiwa ni pamoja na kurejesha vituo vya kujiandikisha kwa ajili ya kupiga kura ili kuhakikisha wanaitumia haki yao ya kikatiba katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwezi Novemba mwaka huu pamoja na Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Alisema kuwa kwa kutambua uzito wa suala hilo, Baraza la Uongozi la TLS limeunda kamati maalum ya kuchunguza na kufuatilia kwa karibu mgogoro wa Ngorongoro, ikijumuisha wanasheria wabobevu aliowataja kuwa ni Dk. Rugemeleza Nshala, Tike Mwambipile, Bumi Mwaisaka, Laetitia Ntagazwa na Paul Kisabo.

Kwa mujibu wa Rais huyo wa TLS, kamati hiyo imepewa jukumu kadhaa, ikiwamo kufanya mashauriano na taasisi mbalimbali pamoja na kutembelea maeneo yenye migogoro, ili kufahamu uhalisia wa hali hiyo, kupitia sera, sheria na mazoea yanayohusiana na umiliki wa ardhi kwa wazawa na kuhakikisha haki za msingi za raia zinazingatiwa kwa mujibu wa katiba, sera na sheria za nchi.

Kamati hiyo pia itaandaa kongamano la kitaifa kuangazia namna bora ya kusimamia maendeleo huku ikilinda haki za wazawa katika ardhi zao za asili na kuchunguza mashauri na hatua zilizochukuliwa kisheria ili kubaini kama kweli kuna watu waliokubali kuondoka kwa hiyari na wale waliokataa kuondoka kutoka kwenye ardhi yao ya asili.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) pia kimeitaka serikali kusikiliza wananchi wa eneo hilo kwa lengo la kupata ufumbuzi wa kudumu na kuepuka maafa.

Pia kimeitaka Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) kurejesha majina ya wapigakura hao katika Daftari la Kudumu la Wapigakura.

HABARI KITAIFA



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (wa tatu kulia), akisikiliza maelezo ya uzalishaji wa mbolea kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Minjingu Mines and Fertilizers, Pardeep Sing Hans, wakati wa mkutano wa biashara na uwekezaji wa USAID Afrika, jijini Dar es Salaam jana. Habari Uk. 8 PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE

# Prof. Janabi: Inachukua miaka 10 hadi 15 kutambua una kisukari

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, amesema mtu anaweza kutambua dalili tofauti mwilini mwake kwa takribani miaka 10 hadi 15 kabla ya kuugua kisukari.

Prof. Janabi ambaye ni Mhadhiri Mshiriki wa Chuo Kikuu cha Magonjwa ya Moyo cha Marekani (FACC), anatoa darasa hilo katika kitabu chake cha 'Mtindo wa Maisha na Afya Yako'.

Anasema kuna hatua za awali kutoka kuwa na ukinzani wa insulini mpaka kupata ugonjwa wa kisukari kamili, na iwapo mtu akizibaini ndani ya miaka hiyo, ataepuka ugonjwa huo.

"Yapo magonjwa ambayo ni kiashiria dhahiri kwamba kuna tatizo la ukinzani wa insulini mwilini. Magonjwa hayo yanatajwa kuwa ni hatua moja kabla ya mtu kuugua kisukari aina ya pili.

"Hii ina maana kwamba, kama hatua zingelichuliwa kukabiliana na chanzo chake, basi mgonjwa asingefika hatua ya kuugua kisukari kamili.

"Inachukua takribani miaka 10-15 kutoka kuwa na ukinzani wa insulini mpaka kupata ugonjwa wa kisukari kamili," anasema bingwa mbobezi wa magonjwa ya moyo.

Anasema kuwa mara zote, chanzo kikuu cha hali hiyo ni ulaji wa mara kwa mara wa vyakula vyenye wanga kwa mwingi (high carb diet) kwa siku, utumiaji sukari na vyakula au vitu vyenye sukari nyingi kama vile soda, keki, pipi na vingine.

Prof. Janabi afafanua kwamba, vyakula hivyo hutibua homoni nyingine zote kwa kuleta hali isiyokuwa na ulinganifu.

"Insulini inavuruga mwili kutoka katika utimamu wake wa afya. Hii ni orodha ya magonjwa yanayosababishwa na ukinzani; uzito mkubwa (obesity), shinikizo la juu la damu (hypertension) na kisukari (diabetes).

"Saratani (cancer); afya ya akili (dementia); magonjwa ya moyo (heart diseases); magonjwa ya figo (kidney diseases); upungufu wa nguvu za kiume; magonjwa ya viungo (arthritis) na upungufu wa hamu ya tendo la ndoa (reduced libido).

"Zamani watu walikuwa wanaishi mpaka miaka 100, lakini bado wako sawasawa kiakili. Pia walikuwa wanaweza kufanya mambo yao wenyewe bila matatizo.

"Siku hizi watu wenye umri wa miaka 65 au 70 wanashindwa kabisa kuendesha maisha, waona wanapoteza uwezo wa kutambua vitu hivyo kwa kuathiri mtumo wa maisha yao ya kila siku, kwa sababu akili zao haziko timamu tena kama awali kwa sababu ya mtindo wa ulaji."


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA MWANZA NA SHINYANGA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza mzunguko wa tatu unaanza kufanyika tarehe 21 hadi 27, Agosti, 2024 katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga kwa siku saba kwa kila kituo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 21 na kuhitimishwa Jumanne tarehe 27 Agosti, 2024.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 9 na kubonyeza.Kisha atachagua Namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***

**Limetolewa tarehe 16 Agosti, 2024 na:**

**Kailima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**


# Washindi wa kampeni ya NBC wakabidhiwa zawadi za milioni 40/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imekabidhi zawadi zenye jumla ya Sh. milioni 40 kwa washindi wa kampeni yake ya 'Shinda Mechi Zako Kinamna Yako' inayolenga kuchochea ukuaji uchumi miongoni mwa wateja wake kupitia uwekaji akiba.

Jumla ya washindi 45 wamepatikana katika kipindi cha miezi mitatu ya kampeni hiyo ya mwaka mmoja kupitia droo za kila mwezi zilizofanyika makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam, zikihusisha maofisa wa benki hiyo pamoja na wawakilishi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nchini.

Kupitia kampeni hiyo inayolenga makundi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi ambao ni wateja wa benki hiyo, wakiwamo wateja binafsi, waajiriwa, wamiliki wa biashara ndogo na wanafunzi, ilishuhudiwa washindi wakiibuka na zawadi mbalimbali ikiwa ni pamoja na fedha taslimu, simu za mikononi, kompyuta mpakato, friji, vishkwambi vya watoto, bima za afya na majiko ya kisasa ya kupikia.

"Pamoja na zawadi hizo, mwisho wa mwezi huu (Agosti) tunatarajia kutoa zawadi ya gari moja aina BMW X1 ambalo ni kati ya magari mawili tuliyopanga kutoa kama zawadi kuu katika kampeni itakayodumu kwa kipindi chote cha mwaka huu," alisema Moses Senkoro, Mtaalamu wa Masoko Benki ya NBC, wakati akitoa tathmini ya miezi mitatu ya kampeni hiyo inayohamasisha tabia ya uwekaji akiba miongoni mwa Watanzania kupitia taasisi zilizo rasmi.

Akizungumzia droo hizo zinazofanyika kila mwezi, Senkoro alisema zinahusisha wateja wote waliokidhi vigezo na masharti wanaohudumiwa na benki hiyo kupitia huduma zake mbalimbali.

Meneja Masoko wa Benki hiyo, Arina Kimaryo, aliwataka wateja mbalimbali wa benki hiyo, hususani vijana, kutumia vyema fursa hiyo iliyotolewa na benki hiyo kupitia kampeni hiyo ili wanufaike kupitia zawadi mbalimbali zinazoambatana na kampeni hiyo.

"Tunaposema shinda mechi zako kupitia kampeni hii, tunalenga kuitumia falsafa ya mchezo wa soka ambayo Benki ya NBC ndio wadhamini wakuu wa ligi tatu muhimu hapa nchini, ikiwamo Ligi ya Kuu ya NBC.

"Tunaingiza falsafa hiyo kwenye maisha tukiamini kwamba wateja wetu wana ndoto, malengo na maazimio mbalimbali waliyopanga kufanikisha hususani kiuchumi na kijamii, ikiwamo ujenzi, kukuza biashara zao, kusomesha watoto na mengine mengi. Kupitia kampeni hii tunalenga kuwasaidia kufanikisha hilo," alisema.

## Kizimbani mashtaka ya kuingilia mfumo wa matokeo UDSM, IFM

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Arusha, James Fundi na mwenzake, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kwa tuhuma za kuingilia mfumo wa kompyuta wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya kwa lengo la kubadili matokeo.

Inadaiwa mshtakiwa Fundi kupitia mfumo wa kompyuta, pia aliingilia mfumo wa matokeo ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM).

Mbali na Fundi, mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni mkazi wa Tanga, Ramadhani Mningo ambao walisomewa mashtaka yao juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Godfrey Mhini, wa mahakama hiyo na Wakili wa Serikali Shinday Michael.

Akisoma hati ya mashtaka, Michael alidai katika tarehe na mwezi visivyofahamika, mwaka huu, ndani ya Tanzania, washtakiwa hao kwa nia ovu, walikula njama ya kuingilia mfumo wa kompyuta wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya kwa lengo la kubadili matokeo.

Alidai kuwa Febrauri 17, 2024, mshtakiwa Fundi alisambaza taarifa za uongo kwa njia ya mtandao wa WhatsApp, akituma ujumbe uliosomeka 'Muhimu; tunatoa huduma ya kubadili matokeo katika mifumo ya matokeo kwa levels za University, Colleges, Advanced Level & O level pamoja na kufuta madeni.

"Karibu kubadili matokeo kwa system za online pamoja na huduma ya kufuta madeni katika system tofauti tofauti, tunabadili grade kwa mfumo wa online, huduma zetu ni uhakika malipo baada ya kubadili.

'Tunapandisha GPA, tunabadili grade kwa kupandisha grade points na credit point kwa Sh. 50,000, carry Sh. 60,000, Re take Sh. 80,000, Disco Sh. 250,000, GPA upgrade Sh. 250,000, A level division Sh. 300,000, O level Sh. 250,000, kufuta deni la ada asilimia 40 ya deni.

"Bei zinapanda kulingana na uhitaji sokoni, hivyo zitazidi kupanda. Bei ya kazi ni makubaliano, forward ujumbe huu kusaidia wahitaji."

Pia alidai mshtakiwa Fundi alituma ujumbe huo katika group la WhatsApp la Chuo Kikuu Mzumbe 2020/21, CBE Dar es Salaam, CBE Dodoma na IFM.


Aliendelea kudai kuwa Julai 22, 2024, sehemu isiyofahamika ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mshtakiwa huyo isivyo halali, kupitia mfumo wa kompyuta aliingilia mfumo wa matokeo ya wanafunzi wa UDSM na IFM.

Mshtakiwa huyo anakabiliwa na mashtaka ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu Sh. 514,500 kutoka kwa watu mbalimbali kwa madai kwamba angewabadilishia matokeo yao ya vyuo.

Kwa upande wa mshtakiwa Mningo, inadaiwa kwamba katika tarehe tofauti mwaka huu, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alijipatia Sh. 110,000 kutoka kwa watu mbalimbali, akidai kwamba angewabadilishia matokeo ya vyuo wakati akijua si kweli.

Inadauwa kuwa, Julai 27, 2024, Mtaa wa Amani, Arusha, Fundi alitumia laini ya simu ya Gift Kambonge, bila kutoa taarifa kwa mtoahuduma huku mshtakiwa Mningo akidaiwa kutumia laini ya simu ya Aisha Athumani na Mwajuma Mbwana bila kutoa taarifa kwa mtoahuduma.

Baada ya kusomewa mashtaka yao, walikana mashtaka yote, upande wa Jamhuri ulidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kesi iliahirishwa hadi Septemba 2, mwaka huu kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa hao hoja za awali.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (katikati), akishuhudia wakati Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Hassan Saidy (kushoto), akibadilishana makabrasha na Kiongozi wa kampuni ya Drem Group Ltd, Mhandisi Idd Bakari, jijini Dodoma jana, baada ya kutiliana saini mikataba ya miradi ya kuweka umeme katika vitongoji 3,060 sawa na vitongoji 15 kila jimbo, itakayogharimu Sh. bilioni 360. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

TAMASHA LA KIZIMKAZI

# NMB yamkabidhi Samia skuli ya mil. 800/-

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amekabidhiwa na kuzindua Skuli ya Maandalizi iliyopewa jina lake, iliyoko Kijiji cha Tasani, Makunduchi, Zanzibar, iliyojengwa na Benki ya NMB kwa gharama ya Sh. milioni 800.

Jiwe la msingi la ujenzi wa Skuli ya Dk. Samia Suluhu Hassani liliwekwa Agosti 29, 2023 na Rais Samia mwenyewe wakati wa Tamasha la Kizimkazi mwaka jana, NMB ilitarajia ingegharimu Sh. milioni 600, lakini kutokana na kuongezeka kwa maeneo ya ujenzi na samani za ndani, skuli hiyo imekamilika ikigharimu Sh. milioni 800.

Akipokea na kuzindua skuli hiyo jana, Rais Samia alikiri kuvutiwa si tu na ufadhili wa NMB kujenga shule hiyo, bali mchango wa jumla wa taasisi hiyo katika Tamasha la Kizimkazi 2024, ambapo imefanya mambo mengi na makubwa ikiwamo uzinduzi wa miradi mbalimbali na kufichua kuwa serikali yake inategemea kwa kiwango kikubwa kuwapo benki hiyo kama mdau kinara wa maendeleo.

"Tunaishukuru sana NMB si tu kwa hili, bali kwa ujumla wake, imetoa mchango mkubwa katika Kizimkazi Festival, kama ambavyo Ofisa Mtendaji Mkuu alivyobainisha, wamefanya makubwa sana, kote Wilaya ya Kusini kuna miradi yao inayofanana na huu. Ninataka niseme serikali tunategemea sana kuwapo kwao kwa ajili ya usaidizi wao.

"Mbali na kazi kubwa waliyofanya katika mradi huu na waliyofanya kwenye tamasha hili kwa ujumla, zaidi niwapongeze kwa kutambuliwa kimataifa na kupewa tuzo mbalimbali, zikiwamo mlizopewa na Jarida la Euromoney.

"Nimesoma 'article' za Euromoney ikiwatambua NMB kuwa ndio Benki Bora Tanzania na pia ndio Benki Inayojali makazi, jamii na utawala bora, na kupitia skuli hii ni sehemu ya mfano hai wa uwajibikaji wao kwa jamii.

"Wanafanya hivi kwa sababu jamii ndio iliyowafikisha walipo, wanapata faida kubwa na kutenga fungu la kurejesha kwa jamii hiyo.

"NMB wangeweza kukaa na faida yao yote, lakini kwa kujali kwao, wamechagua kurejesha kwa jamii siyo tu ya Wazanzibar bali ni kwa Watanzania wote. Ninatamani taasisi zingine zingefuata nyayo za NMB katika kuitumikia jamii kupitia faida wanazopata," alisema Rais Samia.

Awali Rais Samia alisema skuli hiyo ni zao la kaulimbiu ya Kizimkazi Festival 2023 ya 'Tuwalinde Watoto Wetu kwa Maslahi ya Taifa' na kwamba ujenzi wa shule bora na ya kisasa uliofanywa na NMB unatekeleza kwa vitendo Sera ya Afya ya Uzazi inayozingatia makuzi sahihi na ustawi watoto katika siku 1,000 za awali tangu kuzaliwa hadi wanapoanza elimu ya awali.

Akikabidhi skuli hiyo kwa Rais Samia, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema wanayo furaha kubwa kukamilisha kwa wakati ujenzi wake na kuipa jina la Rais.

Ruth alibainisha kuwa, gharama ya Sh. milioni 800 zimejumuisha ongezeko la ujenzi wa sehemu ya chakula, ununuzi wa samani kwa ajili ya walimu na wanafunzi, uwekaji viyoyozi katika ofisi ya walimu, sehemu ya paredi na sehemu ya kuchezea watoto, zikiwamo bembea.

"Ongezeko hilo la thamani limetokana na ujenzi huo wa ziada ambao haukuwa katika mpango wa awali uliojumuisha madarasa matano, ofisi ya mwalimu mkuu, ofisi ya walimu, stoo na miundombinu ya majisafi na majitaka, lakini kwa kutambua umuhimu wa vitu vilivyoongezwa, tukaona ni vyema kuongeza gharama hizo ili kufanya shule hiii iwe na viwango bora vinavyohitajika kwa ajili ya watoto wetu.

"Kwetu sisi NMB, skuli hii ni alama ya matumaini na ndoto mpya kwa watoto wa eneo hili, ambao watajengewa msingi imara wa elimu, tukiamini kuwa kupitia elimu, tunaweza kuleta mabadiliko makubwa katika jamii yetu na kuandaa viongozi wa kesho wenye uadilifu, maarifa, uzalendo," alisema Ruth.

Aliongeza kwamba mradi huo unaotokana na sera ya NMB ya "Uwajibikaji kwa Jamii" hivyo ni mwendelezo wa mchango wao mkubwa waliotoa katika sekta za elimu, afya, usaidizi wa changamoto za majanga na vifaa saidizi vya watu wenye ulemavu huku akichanganua kwa kutaja mambo iliyofanya katika nyanja zote.

"Benki yetu inatenga asimilia moja ya faida yake baada ya kodi ili kusaidia sekta hizo za kimkakati, ambapo tangu Januari hadi Juni mwaka huu, tumeboresha mazingira ya shule mbalimbali za serikali za Bara na visiwani Zanzibar, kwa kutoa madawati, viti na meza za walimu na kuezeka madarasa.

"Vilevile, tumetoa zaidi ya madawati 6,420 kwa shule 103 na kuwezesha zaidi ya wanafunzi 19,000 kujifunza wakiwa wameketi kwenye madawati, lakini pia tumetoa meza 64 na viti 88 kwa ajili ya walimu ili kuboresha mazingira ya utoaji elimu," alisema Ruth.

Aliongeza kwamba, benki yake imesaidia skuli tisa vitanda zaidi ya 360 vya kulalia wanafunzi 720, hasa kwa watoto wa kike, huku kupitia NMB Foundation, ambayo ni asasi isiyo ya kibiashara ya benki hiyo, wanasomesha vijana wa Kitanzania 130 katika vyuo vikuu mbalimbali nchini.

Kuhusu ujenzi wa Shule Maalum mkoani Dodoma, Ruth alisema: "Mwaka Jana wakati wa Sherehe za Miaka 25 ya NMB, tulikuahidi kujenga shule maalum yenye thamani ya Sh. bilioni 2.5.

"Mheshimiwa Rais, ninapenda kukufahamisha kuwa maandalizi yameanza, eneo tumeshaoneshwa pa kujenga huko Bahi, Dodoma na nikuhakikishie kwamba ujenzi unaanza mara moja."

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanawake jitokezeni kugombea uongozi

**KIPENGA** cha kuanza kwa mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa kimeshapulizwa na Tume Huru ya Uchaguzi imeshatangaza kuwa uchaguzi huo utafanyika mwezi Novemba mwaka huu.

Wakati mchakato huo ukianza, rai yetu ni kwa wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi badala ya wao kubaki kuwa wapigakura wa kuwachagua wengine.

Huu ni wakati wa kuonesha kuwa wanawake wanaweza kupambana na kushinda kwenye uchaguzi kutokana na watakavyoweza kujieleza na kumwaga sera zao.

Hata hivyo, kuna baadhi ya wanawake hukatishwa tamaa kugombea nafasi za uongozi kisiasa kutokana na vikwazo wanavyokumbana navyo.

Wengine wanakosa ujasiri wa kuthubutu baada ya kuona wenzao wanavyopata misukosuko ikiwamo kudhalilishwa na kutukanwa kwenye majukwaa.

Hali hiyo inathibitishwa na baadhi ya viongozi wanawake waliowahi kushika nyadhifa za juu serikalini na kwenye taasisi mbalimbali, mikikimikiki waliyopambana nayo mpaka kufanikiwa kushika uongozi.

Miongoni mwa sababu zinazowadhoofisha wanawake wengi kujitokeza kuwania nafasi iwe kwenye siasa au taasisi ni kuombwa rushwa ya ngono.

Kuna wanawake wanaojitambua ambao wakishatajiwa suala la rushwa ya ngono, anaona isiwe tabu na kuamua kuendelea na mambo mengine. Sehemu yoyote linapokuja suala la kupewa nafasi kwa upendeleo, ufanisi hukosekana kwasababu ya kukosekana heshima.

Hii ni vita kubwa na inapaswa kukomeshwa na wanawake wenyewe kwa kujitambua na kutokubali kudhalilishwa kwa namna yoyote ile.

Kwenye nafasi za kisiasa, wanawake wengi hulalamika kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji kwa kuitwa majina ya ajabu ajabu ili tu wakatishwe tamaa.

Kwa wanawake walio kwenye ndoa wanakuwa kwenye mtihani mkubwa baada ya wenza wao kusikia yanayofanyika kwenye mchakato wa kuwania nafasi hizo na kuamua kuwakataza ili kuepuka kashfa.

Suala hili linahitaji kukemewa na pia elimu ya kutosha kuanzia mijini na vijijini ili wanawake wengi waelimike na kujitokeza kuwania nafasi.

Vyama vya siasa, wanaharakati wa haki za binadamu mna kazi kubwa ya kutoa elimu kupiga vita jambo hilo.

Kwa kudhoofisha wanawake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi, kunaweza kukapoteza ari yao ya kuonyesha vipaji vyao vya uongozi.

Na katika maeneo mengi ya kazi imeshuhudiwa kuwa wanawake wanapopewa uongozi wanafanya vizuri na hata suala la rushwa ya ngono huwezi kulisikia.

Mapambano ya rushwa ya ngono ni lazima yawe makubwa ili kukomesha hali hiyo kabisa.

Aidha, wanawake wajitahidi kuhamasishana wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali wasibakie kuwa wapigakura.

Katiba inaruhusu kugombea, kupiga kura na kupigiwa, lakini bado hawajitokeza kwa hofu ya udhalilishaji.


"Vikwazo vipo vingi vinavyowafanya wanawake washindwe kujitokeza kugombea, sababu moja wapo hatuna uthubutu, pili, elimu ya uraia haiwafikii kinamama nje ya miji, juhudi zifanyike wafikiwe. Rushwa ya ngono ni kikwazo, waume zetu wakisikia unataka kugombea wanakukataza kama haujaolewa wazazi wanakukataza kugombea," anasema aliyewahi kuwa waziri wa zamani Shamim Khan.

Mwanamke akitaka kugombea nafasi yoyote anapaswa kukataa rushwa ya ngono na akiwa na heshima yake hakuna atakayemfuata.

Pia ni muhimu wakajua kanuni na vyama vya siasa vifanye bidii kupeleka kanuni hizo hadi ngazi ya chini ndipo watapatikana wanawake wengi.

Kuna nafasi za viti maalum vya udiwani na ubunge, ambazo zimependekezwa na wadau wa siasa ziwe na ukomo wa miaka kumi ili kutoa nafasi kwa wanawake wengine kuziwania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanasiasa waoneshe vitendo si blah blah

Na Mwandishi Wetu

**KATIKA** kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu na mkuu 2025, tumeanza kuwaona watia nia na viongozi wakiwatembelea wapigakura.

Wamekuwa 'wakipigana vikumbo' majimboni, kwenye kata na hata mitaani kujionesha ili kutetea au kuomba kuchaguliwa tena.

Viongozi hao wakiwamo wa kitaifa, serikali za mitaa, wilaya, wabunge na madiwani wanataka kuomba kura ili waendelee na kazi, wanatumia muda mwingi kujieleza kwa wananchi walivyotekeleza baadhi ya miradi.

Wengi wao wamekuwa wakitumia muda huo, kueleza jinsi watakavyofanikisha miradi ambayo bado haijaanza kujengwa kabla ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), haijapuliza kipenga cha uchaguzi wa sasa na wa mwakani.

Huku wakikumbuka ya kwamba, miradi hiyo ikiwamo ujenzi wa barabara, masoko na kero ya upatikanaji maji na umeme kwa wananchi kwa baadhi ya maeneo imebaki kuwa mwiba mchungu kwa wapigakura dhidi ya wawakilishi hao.

Wanatarajiwa waoneshe nia, kutupa karata nyingine ili wachaguliwe tena kutokana na maswali wanayokumbana nayo kwenye mikutano yao ya hadhara.

Maswali hayo si utani yanaonesha jinsi wananchi walivyokata tamaa kuhusu kile walichokitarajia katika miaka mitano ya uongozi wao.

Mathalani, huduma za kijamii kama upatikanaji wa uhakika wa maji, miundombinu ya elimu na vifaa kama madawati, barabara, madaraja na zahanati zenye dawa, wataalamu na vifaa tiba, ambazo bado ni tatizo.

Badala yake viongozi hao wa kisiasa kwa nyakati tofauti, wanaahidi kuwa kazi zitafanyika kabla ya kuanza kwa michakato ya uchaguzi.

Ni mambo yanayojidhihirisha wakati wananchi wakihoji maswali na kuwakumbusha viongozi hao kwa kuwataja majina na mlolongo wa ziara zao katika maeneo yao na mikutano waliyofanya kwa nyakati tofauti.

Wapigakura wanawaambia kuwa, wanachoona ni changa la macho kwani kukamilika kwa miradi hiyo na kupatikana huduma bora za kijamii kumekuwa ndoto.

Wananchi katika kudhihirisha hilo, wamediriki hata kuwatamkia baadhi ya wanasiasa hisia zao mubashara na kuhoji kwa nini hawawahitaji tena.

Wanasema ni kushindwa kutimiza ahadi walizotoa kabla ya uchaguzi na sasa wanataka tena kuchaguliwa?

Wanaona kuwa, kinachoendelea ni kuwalaghai ili wawachague tena kwenye uchaguzi unaokuja.

Katika utetezi wao, wamekuwa wakisisitiza utekelezaji wa miradi katika maeneo mbalimbali unategemea na mgao wa fedha kutokana serikali kuu.

Wanasema serikali inatoa fedha hizo kutoka kwenye bajeti kila mwaka wa fedha kulingana na mgawanyo maalumu.

Kana kwamba haitoshi, wamekuwa wakiwasimamisha wataalamu kutoka wizara mbalimbali kujibu maswali kuhusiana na kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo.

Pamoja na wataalamu hao kutumika kama nyenzo ya kutetea hoja zao, bado wanagonga mwamba kutokana na wapigakura kueleza waziwazi kutoafikiana nao kwa kuamini kwamba ni mambo ya ahadi hewa.

Sababu nyingine ya kuamini kuwa ni ahadi hewa ni kitendo cha wataalamu na wahandisi kuonekana kwenye maeneo ya miradi kufanya vipimo na kutoweka.

Wanarejea tana viongozi wengine wanapotembelea sehemu hizo kana kwamba wanakwenda kufanya ukaguzi.

Baada ya kufanya ukaguzi huo na kuzungumza na wananchi, viongozi hao wakiondoka na wataalamu nao wanatoweka hadi wakati mwingine tena viongozi hao na wengine wanapopanga ziara nyingine kwa minajili ya kukagua.

Wanapofika wanapigwa na butwaa huku wakiwabana wataalamu kutoa majibu ambayo wananchi hawaridhiki nayo na kusababisha wagune, kuzomea na kutamka wazi kuwa hawataki tena ahadi hewa.

Wanasiasa hali hiyo inadhihirisha ni namna gani wananchi wameamka kwa kuthibitisha hawako tayari kuendelea kudanganywa kwa maneno, bali wanachotaka kuona ni vitendo ili maeneo yao yawe na maendeleo.

Wananchi wanapenda kuona umeme unawaka kwenye nyumba zao, maji yanapatikana muda wote, barabara zinapatikana ili kuwa na uhakika wa usafiri, elimu kwa watoto wao na afya bila vikwazo vyovyote.

# Mwinyi, Balozi India waahidi kuinua uchumi wa Zanzibar

**Na Mwandishi Maalum,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema miongoni mwa mafanikio makubwa inayojivunia kutokana na ushirikiano wa diplomasia uliopo kati yake na Serikali ya India ni kuanzishwa kwa tawi la Chuo Kikuu cha Teknolojia cha IIT Madras, Zanzibar.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar alipozungumza na Balozi wa India nchini, Shri Bishwadip Dey aliyefika kujitambulisha.

Alisema Chuo Kikuu cha Teknolojia cha IIT Madras ni fursa muhimu kwa sekta ya elimu Zanzibar itakayoleta mageuzi makubwa ya mifumo na kukuza teknolojia nchini.

Dk. Mwinyi alimhakikishia balozi huyo ushirikiano mzuri uliopo baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na chuo hicho kwa kushirikiana na Serikali ya India ni jitihada zao za kuimarisha uhusiano wa diplomasia baina yao.

Alisema India imekua mdau mkubwa kwa maendeleo ya Zanzibar kupitia sekta mbalimbali, ikiwamo miradi mikubwa ya majisafi na salama, sekta za afya na elimu ambapo imekuwa ikishirikiana kwa miaka mingi.

Hivyo, aliomba India kupitia teknolojia kubwa waliyonayo na kwa weledi wa mitandao ya kijamii iliyobobea, kuendelea kuitangaza Zanzibar kimataifa kupitia tawi la chuo hicho duniani pamoja na sekta za biashara na uwekezaji.

Dk. Mwinyi alisema sekta za afya na elimu zimepata ushirikiano mzuri kutoka India kwa kuendelea kuwapokea Watanzania wengi kwa matibabu nchini humo sambamba na Watanzania wanaoendeleza masomo yao pamoja na ushirikiano wa biashara uliopo baina ya pande mbili za ushirikiano.

Akizungumzia sekta ya utalii ikiwa ni sekta kiongozi ya uchumi wa Zanzibar, Rais Dk. Mwinyi alimwomba balozi huyo kuangalia uwezekano wa kuongeza watalii wengi wa India, alimweleza kuwa watalii wengi wanaoingia Zanzibar ni kutoka Ulaya Mashariki na kwingineko duniani.

Balozi Shri Bishwadip alimhakikishia Rais Dk. Mwinyi kuendeleza historia ya ushirikiano uliopo wa pande mbili hizo hasa kwenye kuboresha sekta za biashara, uchumi, utalii na uwekezaji.

Balozi huyo pia alimwahidi Rais Dk. Mwinyi kuendelea kupokea wafanyabiashara wakubwa kutoka India, wenye nia ya kuwekeza Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Chuo cha IIT Madsa kilianzishwa Zanzibar mwezi Oktoba mwaka jana kwa ushirikiano wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya India. Chuo hicho kinatarajiwa kuleta mageuzi makubwa kwenye sekta ya elimu Zanzibar hasa kutoa fursa kwa wazawa ya kujifunza teknolojia.

Uhusiano wa diplomasia baina ya Tanzania na India ni wa historia ambapo India ilifungua ubalozi wake Dar es Salaam mwezi Novemba mwaka 1962 na mwaka 1974 ikafungua ubalozi mdogo Zanzibar. Uhusiano wa pande mbili hizo umeendelea kuimarika kwa fursa nyingi za biashara na maendeleo kupatikana.



Mkurugenzi Mtendaji wa I&M Group Plc, Sarit Raja Shah (katikati), akipongezana na Ofisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya I&M Tanzania, Zahid Mustafa, wakati wa sherehe za maadhimisho ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa benki hiyo nchini Kenya na uzinduzi wa ofisi za makao makuu ya I&M Masaki, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa I&M Group Kikanda, Kihara Maina. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hatima kesi ya Kabendera, Vodacom leo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masjala Ndogo Dar es Salaam leo inatarajia kutoa uamuzi kama shauri la madai lililofunguliwa na mwanahabari Erick Kabendera akiomba kampuni ya mawasiliano ya Vodacom Tanzania iamuliwe kumlipa Sh. bilioni 28 kwa madai ilifanikisha kutekwa kwake, iko mahakamani kihalali au la.

Uamuzi huo unatarajiwa kutolewa leo mbele ya Jaji Salma Maghimbi anayesikiliza shauri hilo.

Julai 9, mwaka huu, akimwakilisha Kabendera, Wakili Peter Madereka alidai kuwa, walalamikiwa Vodacom Tanzania kupitia Wakili wao, Gasper Nyika, waliwasilisha majibu ya madai dhidi yao pamoja na kusudi la kupinga madai yaliyoko mahakamani.

Wakili Nyika alidai waliwasilisha majibu ya utetezi pamoja na pingamizi, walikubali pingamizi walilowasilisha lisikilizwe kwa njia ya maandishi.

Jaji Maghimbi aliamuru upande wa wajibu maombi kuwasilisha hoja za pingamizi Julai 23 mwaka huu.

Mwombaji alitakiwa kujibu pingamizi hilo Agosti 6 mwaka huu, kama kuna hoja za nyongeza zilitakiwa kuwasilishwa Agosti 13, mwaka huu na mahakama inatarajia kutoa uamuzi kama shauri hilo liko mahakamani kihalali au la leo.

Vodacom kupitia Wakili Nyika wanapinga shauri hilo kusikilizwa kwa madai kuwa, kesi ilifunguliwa nje ya muda kisheria, hivyo wanaomba itupwe.

Katika kesi ya msingi, Kabendera anaomba mahakama hiyo iiamuru kampuni hiyo imlipe fidia ya Dola za Marekani 10 milioni (sawa na Sh. bilioni 28 ), akiituhumu kuwa ndio iliyofanikisha kukamatwa kwake na askari polisi, tukio analoliita kutekwa na kisha kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi mwaka 2019.

Kabendera anadai kuwa kutokana na matukio hayo, amepata madhara ya kiuchumi na yasiyo ya kiuchumi, ya kijamii, maumivu ya kiakili na kimaono, hasara ya kutokufurahia maisha, hasara ya maendeleo binafsi na hadhi yake katika jamii na kutokuaminiwa kitaaluma.

Kabendera anataka kampuni hiyo imlipe Dola za Marekani milioni 10 kama fidia ya hasara halisi na riba kwa kiwango cha mahakama kuanzia tarehe ya hukumu mpaka kumaliza malipo yote.

Pia anataka alipwe fidia ya hasara ya jumla kadri mahakama itakavyotathmini, gharama za kesi na nafuu nyingine kadri mahakama itakavyoona inafaa.

Kwa mujibu wa hati ya madai katika kesi hiyo, Kabendera anaeleza matukio yaliyojiri katika simu yake kabla ya tukio la kukamatwa kwake, kuwa ilianza kupoteza mawasiliano na kumfanya ashindwe kupata huduma ya mawasiliano.

Kabendera pia ameelezea juhudi alizofanya kujua chanzo cha hali hiyo kwa kufanya mawasiliano na mwakilishi wa huduma kwa wateja na hata kutembelea ofisi za kampuni hiyo, lakini hakupata ufumbuzi wa tatizo hilo.

Katika hati ya madai, Kabendera anadai kuwa Julai 27, 2019, saa tisa alasiri, alipowasha simu yake ambayo alikuwa ameizima usiku wa siku iliyopita, ndipo alipobaini kuwa haikuwa na mtandao.

Anadai kuwa mwakilishi wa huduma kwa wateja wa Vodacom alimweleza kuwa namba yake ya simu ya Vodacom (+255767456796) ilikuwa na changamoto za kiufundi ambayo ilimhitaji kutoa taarifa katika kituo cha huduma kwa wateja cha karibu kilichoko Tegeta.

Kabendera alimtaka mwakilishi huyo kuelezea tatizo ni nini kabla ya kwenda kituoni huko, lakini mwakilishi huyo alikataa, akidai kuwa ni suala nyeti ambalo linamtaka aende binafsi kituoni huko.

Badala yake walimshauri atembelee ofisi zao zilizoko Mlimani City asubuhi hiyo, hata hivyo saa tisa alasiri siku hiyohiyo ya Julai 29, 2019, ghafla simu yake ilianza kufanya kazi, kisha alipigiwa simu na mwakilishi wa Vodacom ambaye alimtaka (Kabendera) amwelezee tatizo lake na baada ya Kabendera kumwelezea kwa takribani dakika tatu, alikata simu akiahidi kumpigia baadaye kidogo.

Anadai kuwa baada ya dakika tatu, alipokea simu iliyopigwa kutoka huduma kwa wateja Vodacom ambayo alipokea, akabaini kuwa ilikuwa ni sauti ya mwanamume, ambaye alimtaka Kabendera aeleze mahali alikokuwa na kwamba simu hiyo ilikuwa ikikwaruza kama vile ilikuwa inarekodiwa.

Anadai kabla ya simu hiyo kukatwa, Kabendera alimsikia aliyempigia simu akinong'ona kuwa alikuwa nyumbani kwake na kuongeza kuwa "sogea karibu na nyumba yake".

Kwa mujibu wa hati hiyo, maelezo hayo yalimshtua Kabendera na akakimbia sehemu ya juu ya nyumba yake ambako aliona magari kadhaa ambayo hakuyafahamu karibu na nyumba yake.

Kisha lilitokea gari lingine aina ya Toyota Alphard lililoegesha mbele ya magari hayo upande wa kulia mwa nyumba yake, wakashuka watu wanne ambao walijitambulisha kuwa maofisa wa Jeshi la Polisi lakini walikataa kutoa vitambulisho. Walimpiga pingu kumshikilia kizuizini kwa siku mbili.

Katika hati hiyo, inadaiwa kuwa wakati wa mahojiano, maofisa wa polisi walifika katika chumba cha mahojiano wakiwa na karatasi zilizochapishwa kutoka katika kompyuta za akaunti za fedha ya simu na namba za simu alizokuwa amezipiga kwa mwaka mzima.

Hivyo, walimhoji lengo la kila muamala aliofanya kwa mwaka mzima na pia uhusiano wake na watu aliokuwa amewasiliana nao miaka kadhaa.

Kabendera analalamika kuwa polisi na serikali walitoa taarifa kadhaa zenye mgogoro kwa umma kuhusiana na anachokiita "kutekwa" kwake na kwamba walimtuhumu kwa kutokuwa raia na kumkashfu Rais (wa wakati huo) John Magufuli.

Anadai alishtakiwa mahakamani kwa makosa ya utakatishaji fedha, uhujumu uchumi na ukwepaji kodi na matokeo yake walimweka chini ya ulinzi mkali katika mahabusu ya Gereza la Segerea.

Inadaiwa katika hati hiyo kuwa wakati akiwa mahabusu, mama yake, Verdiana Mujwahuzi alifariki dunia na hakuruhusiwa kuhudhuria mazishi yake na kwamba hata yeye mwenyewe alikuwa na tatizo kiafya.

Anadai katika hati hiyo kuwa kutokana na hali hiyo, aliamua kukiri makosa na kulipa fidia ya Sh. milioni 273 ili atoke mahabusu na kwamba baada ya kuachiliwa marafiki na familia yake walimweleza kuwa walipigiwa simu na polisi wakiwaonya kutokumtembelea mahabusu na kwamba vinginevyo wangepata hatari.

# Marekani yatoa dola milioni 8.3 kwa kampuni nchini

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI ya Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la (USAID), imetangaza kuwekeza Dola za Marekani milioni 8.3 kwa kampuni tisa za Tanzania ili kukuza biashara, kuboresha usalama wa chakula na kuimarisha ushindani wa Tanzania.

Msaada huo utaiwezesha Tanzania kuongeza ushindani katika mauzo ya nje kupitia Mpango wa Ukuaji na Fursa Afrika (AGOA).

Mkurugenzi wa Mipango USAID/Tanzania, Craig Hart, alitangaza hatua hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya maonesho ya shughuli za biashara na uwekezaji ya USAID Afrika ambayo ilihudhuriwa pia na Waziri wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo.

Craig alisema kuwa kampuni tisa za ndani zitapata ruzuku chini ya Mradi wa Biashara na Uwekezaji wa USAID Afrika na alitaja kampuni hizo kuwa ni BioBuu, Biotan Limited, Central Park Bees, Minjingu Mines and Fertilizer Limited, Mount Meru Millers, Red Earth Limited, Sabayi Investments Limited, Tanzania Tooku, Garments Co. Ltd na Mtu wa Tatu (Love Honey).

"Leo tunasherehekea ushirikiano wa USAID na kampuni tisa katika sekta muhimu zikiwamo asali, korosho na nguo. Ushirikiano huu unatarajiwa kuzalisha ajira 2,000, kuongeza dola milioni 42.5 katika mauzo mapya nje ya nchi na kukuza nafasi ya Tanzania kama kitovu cha uchumi wa kanda," alisema.

"Tunafungua njia kwa Tanzania kuwa kikapu cha chakula kikanda, muuzaji nishati nje, na kitovu cha ubunifu unaoendeshwa na vijana, na kupitia AGOA tunasaidia kampuni za kitanzania kupata masoko Marekani," AGOA ni sehemu muhimu ya sera ya kiuchumi ya Marekani na Afrika inayozipa nchi zilizo chini ya Jangwa la Sahara kuuza bila ushuru kwa soko la Marekani kwa zaidi ya bidhaa 1,800," alisema.

Alisema Tanzania imejipanga vyema kupanua uzalishaji wake wa asali kwa kuwa sasa ni nchi ya pili barani Afrika kwa uzalishaji wa asali na muuzaji mkuu wa Ulaya na kuongeza kuwa kampuni ya Man Limited (Upendo Honey) kwa kushirikiana na USAID inalenga kuongeza mauzo ya asali nje ya nchi kwa asilimia 767.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Jafo, alisema mradi wa Biashara na Uwekezaji wa USAID Afrika (ATI) umekuwa chachu katika kukuza uchumi na kuboresha maisha ya watu wa Tanzania.

"Onesho hili la shughuli za mradi wa ATI ni ushuhuda wa dhamira yetu ya pamoja za kufungua fursa kubwa za uchumi wa Tanzania kupitia ongezeko la biashara na uwekezaji kwa kuwawezesha wafanyabiashara na kukuza ubunifu katika sekta muhimu za uchumi wetu," alisema Jafo.

Alisema kupitia shughuli hizo Tanzania imeshuhudia ongezeko la mauzo ya baadhi ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi chini ya usaidizi, uzalishaji wa ajira mpya, na uwezeshaji wa wajasiriamali ambao sasa wanachangia kuimarika kwa uchumi wa nchi.

"Tunapoangalia sekta zinazosaidiwa kupitia Mradi wa ATI, tuna matumaini makubwa kwamba, hata mauzo yetu ya nje chini ya mpango wa AGOA yataongezeka sana wakati mipango yote itakapotekelezwa vyema," alisema.

"Nafahamu mijadala inayoendelea kati ya wizara yangu na USAID kupitia mradi wa ATI wa AGOA na Youth Support, na ikifanikiwa kama ninavyotarajia, wakati ujao tutawaleta walengwa wetu ili kuonyesha mafanikio yao," alisema.

Alisema wakati Tanzania ikisherehekea mafanikio kupitia Mradi wa ATI bado kuna kazi kubwa ya kutumia kikamilifu fursa za biashara na uwekezaji.

Alisema kuna haja ya kuendelea kukuza na kuimarisha uwezo wa uzalishaji na usambazaji ili kukidhi mahitaji ya soko, kupanua kapu la mauzo ya nje kwa kupanua zaidi ya sekta za jadi ili kujumuisha bidhaa zilizoongezwa thamani na zenye viwango vya juu.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA**

**Tarehe: 21/08/2024**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela anawatangazia wananchi, wafanyabiashara, makampuni mbalimbali juu ya mnada wa hadhara. Kwa idhini tuliyopewa na Katibu Mkuu Hazina, tunakusudia kufanya mnada wa hadhara wa mali chakavu (Mali zilizotumika) kama vile magari, pikipiki, samani za ofisi, vifaa vya TEHAMA na Mali mbalimbali n.k siku ya tarehe 30/08/2024 kuanzia saa 4:00 asubuhi katika viwanja vya ofisi za Ujenzi Mtaa wa Bondeni na Bomani. Aidha, baadhi ya mali hizo zimeorodheshwa kwenye jedwali kama ifuatavyo:-

| Aina ya mali | Namba ya Usajili | Hali ya kifaa |
|---|---|---|
| Gari Mitsubishi L200 | STJ 7857 | Halitembei |
| Gari Isuzu 300TDI | STK 321 | Halitembei |
| Gari Isuzu TXD | SM 266 | Halitembei |
| Gari Toyota Hilux | SM 2836 | Halitembei |
| Gari Toyota Hilux | TZJ 2049 | Halitembei |
| Gari Suzuki Samurai | STH 8567 | Halitembei |
| Gari Isuzu 300TDI | STK 334 | Halitembei |
| Pikipiki | Jumla zipo 23 | Hazitembei |
| Samani za Ofisi | | |
| Vifaa vya TEHAMA | | |
| Vifaa mbalimbali | | |

Watu wenye nia ya kununua mali tajwa hapo wanaruhusiwa kutembelea mali hizo zilizopo katika ofisi za Ujenzi na Ofisi za Halmashauri (Bomani).

**Masharti ya Mnada**

i. Mnunuzi anatakiwa kulipa fedha 25% ya bei ya thamani ya mali iliyonunuliwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kitatakiwa kulipwa ndani ya siku kumi na nne (14) na kwamba kinyume na hapo kiasi kilichotolewa hakitarudishwa kwa mnunuzi na kwamba mnada utarudiwa tena.
ii. Ukaguzi wa mali husika utafanyika kabla ya siku ya mnada tokea tarehe 30/08/2024 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana.
iii. Gharama za kubadilisha umiliki (Transfer of ownership), kodi na gharama nyingine zote zitakuwa ni jukumu la Mnunuzi.
iv. Mali itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo.
v. Mnunuzi atawajibika kuondoa/kuchukua mali aliyonunua ndani ya siku saba(7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.

2. Imetolewa na,

**Florah. A. Luhala**
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA**


# Vikundi 3,963 vyaundwa elimu malezi chanya

**Na Mwandishi Wetu,** MBOZI

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau, imeanzisha vikundi 3,963 kwa lengo la kutoa elimu ya malezi chanya kwa jamii ili kukabiliana na tatizo la malezi nchini.

Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Mtoto kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Asha Shame, alisema hayo jana mkoani Songwe wakati akifungua mafunzo ya wajibu wa wazazi na walezi katika malezi na matunzo ya familia kwa maofisa maendeleo ya jamii, maofisa ustawi wa jamii na maofisa elimu kutoka ofisi ya Mkoa wa Songwe, Halmashauri za Ileje, Mbozi na Tunduma.

Alisema serikali imeendelea kutumia majukwaa tofauti yakiwamo ya viongozi wa dini na waandishi wa habari katika kutoa elimu ya wajibu wa wazazi na walezi katika malezi ya watoto na familia.

"Jumla ya viongozi wa dini 109 kutoka katika madhehebu ya Kikristo na Kiislamu (TEC, CCT, BAKWATA, CPCT na SDA) na waumini 35,520 wamefikiwa na elimu hii. Jitihada nyingine ni kuanzishwa kwa vituo vya kulelea watoto mchana vya kijamii ambapo tayari vituo 255 vimeshaanzishwa," alisema.


Shame alisema kupitia utafiti uliofanyika mwaka 2015, ilibainika kuwa wazazi wengi, hasa wa kiume, wamekuwa hawawajibiki katika malezi ya watoto na kusababisha jukumu hilo kubebwa na wazazi wa kike katika maeneo yote ya mjini na vijijini.

Pia, alisema elimu ya malezi kwa wazazi ilionekana kikwazo katika suala la malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto ikiwamo lishe bora, afya, malezi yenye mwitikio, fursa za ujifunzaji na ulinzi na usalama wa mtoto.

Kupitia mafunzo hayo, washiriki wanatarajiwa kutoka na mbinu mbalimbali zitakazowawezesha kuzifikia jamii kuanzia ngazi ya kaya na wadau muhimu katika malezi ya watoto, kupata elimu ya mnyororo chanya wa malezi ya watoto kuanzia kipindi cha utungaji wa mimba mpaka vijana kubalehe na kuandaliwa kwa mpango kazi wa Mkoa wa Songwe kuhusu utekelezaji wa mwongozo wa wajibu wa wazazi na walezi katika malezi na matunzo ya familia.

Mkurugenzi wa Shirika la Tanzania Interfaith Patership (TIP), Asina Shenduli, akitoa salamu za asasi hiyo, alisema kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), wameahidi kushirikiana na serikali katika kuhakikisha elimu ya malezi chanya kwa watoto na familia inatolewa kwa jamii, hususan katika ngazi za chini.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa wa Songwe, Menrad Dimoso, akizungumza kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa, alisema mkoa utaendelea kusimamia utekelezaji wa mafunzo kwa maafisa hao ili jamii ipate elimu hiyo na kusaidia wazazi na walezi kujua wajibu wao katika malezi na matunzo ya familia kwa ustawi wa jamii na taifa.



## TBS yawafikia wajasiriamali, wafanyabiashara wilaya 93

**Na Mwandishi Wetu,** KARATU

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limesema hadi sasa limeshatoa elimu kwa wajasiriamali wadogo na wafanyabiashara katika wilaya 93.

Meneja Uhusiano na Masoko TBS, Gladness Kaseka, alisema hayo juzi wilayani Karatu mkoani Arusha, akisema lengo la shirika hilo ni kutoa elimu kwa umma katika ngazi za wilaya zote nchini.

Alisema wanatoa elimu kuhusu umuhimu wa kununua bidhaa zenye ubora na namna ya kuwasiliana na shirika wanapopata changamoto yoyote.

Aidha, aliwataka wananchi kuhakikisha wanasoma taarifa zinazopatikana katika vifungashio za bidhaa pamoja na muda wa mwisho wa matumizi na kununua bidhaa zilizothibitishwa ubora wake na shirika hilo, ili kuepuka hasara ya kupoteza pesa na kulinda afya zao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na vikundi vya wajasiriamali wanaosindika maziwa na wanaooka mikate wilayani humo, shirika hilo liliwapatia utaratibu wa namna ya kupata alama ya ubora ambayo inatolewa bure.

Katibu wa kikundi kinachojishughulisha na usindikaji wa maziwa, Hoisa Monyo na Katibu wa kikundi cha uokaji mikate, Matilda Shirima waliipongeza TBS kwa kutoa elimu wakisema imewasaidia kufahamu mambo mengi umuhimu ikiwamo viwango vya bidhaa wanazozizalisha.

## Muheza yafikia lengo chanjo dhidi ya Usubi

**Na Steven William,** MUHEZA

WILAYA ya Muheza mkoani Tanga imefikia lengo la kutoa kinga dhidi ya ugonjwa wa usubi kwa zaidi ya wakazi 200,000 katika kampeni iliyofanyika kwa kipindi cha siku saba nyumba hadi nyumba.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mratibu wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele wa wilaya hiyo, Julius Mgeni alisema kuwa wakazi hao 200, 258 walijitokeza kupewa kinga ya Usubi ambao ni miongoni mwa magonjwa hayo kuanzia Agosti 12 hadi 18, mwaka huu.

Mgeni, alisema idadi hiyo ya wakazi hao, imeonesha jinsi chanjo hiyo ilivyopata mafanikio kwa wilaya hiyo kutokana na uhamasishaji mkubwa uliofanyika katika maeneo mbalimbali kupitia matangazo kwa kutumia vipaza sauti na mikutano.

Alisema chanjo hiyo ni mwendelezo wa iliyofanyika Februari mwaka huu. Kila mwaka kinga dhidi ya Usubi hutolewa kwa awamu mbili.

Hivi karibuni, Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Fani Mussa, alikaririwa akiwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kupata kinga hiyo ili kuondokana na athari zinazoweza kusababishwa na ugonjwa huo ikiwemo magonjwa ya minyoo, ngozi na upofu wa macho.

# ACT-Wazalendo kumburuza mahakamani Mchengerwa

**Na Oscar Assenga,** TANGA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema watakwenda mahakamani kufungua kesi ya kupinga uamuzi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ilihali Bunge lilishatoa uamuzi kuwa uchaguzi huo usimamiwe na Tume Huru ya Uchaguzi (INEC).

Agosti 16, mwaka huu, Waziri wa TAMISEMI, Mohammed Mchengerwa, alitangaza tarehe rasmi ya uchaguzi huo kuwa ni Novemba 27 mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibuni na Makamu Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho Tanzania Bara, Is-Haka Mchinjita, wakati akizungumza na wananchi wa Jiji la Tanga katika mkutano wa hadhara uliofanyika eneo la Mabanda ya Papa.

Alisema ziara hiyo ilikuwa na lengo la kuhamasisha wanachama kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 27 mwaka huu.

Mchinjita alisema haiwezekani TAMISEMI kusimamia uchaguzi huo ilihali uamuzi ulishatolewa na Bunge wakielekeza usimamiwe INEC, hivyo watakwenda mahakamani kufungua kesi ya kulipinga hilo.

Alisema: "Nataka niwaambie sisi ACT- Wazalendo, tunajiandaa kufungua kesi wiki hii, tunaipelekea TAMISEMI mahakamani kuishtaki kwa kuwa wana nia ya kusimamia uchaguzi wakati kuna uamuzi ya Bunge ukielekeza INEC".

Alisema wanapokwenda kwenye uchaguzi wananchi watapata fursa ya kuamua ni kina nani waunde Serikali ya Mtaa na Vijiji.

Vilevile alisema licha ya kwamba Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi ya Mwaka 2024, inatoa mamlaka ya kusimamia uchaguzi lakini wameona kuna dalili za TAMISEMI kutaka kupoka mamlaka hayo.

"Serikali kupitia TAMISEMI imeendelea kushikilia msimamo wake wa kutaka kusimamia uchaguzi kwa kuwa hivi karibuni tumemsikia Waziri mwenye dhamana akitangaza tarehe ya kufanyika kwa uchaguzi huo, hivyo chama chetu tumejipanga kufungua kesi kupinga hilo," alisema.

Kadhalika, alisema wamejiandaa kusimamisha wagombea katika vijiji vyote kwenye majimbo 125 ili kuchuana na wagombea kutoka vyama vingine vya siasa.

Pia, alitoa tahadhari kwa viongozi wa upinzani kuunganisha nguvu zao kwa kipindi hiki, kuhakikisha uchaguzi huo na ule wa mwakani wanashinda kwenye nafasi mbalimbali za uongozi.

Alisema kuelekea kwenye uchaguzi huo utakuwa ni kipimo halisi cha kuangalia 4R ikiwamo maridhiano na vyama vya siasa vya upinzani yaliyoazishwa na Rais Samia Suluhu Hassan, tangu alipoingia madarakani.



Mshauri wa Rais na Mwenyekiti wa Kamati ya Jukwaa la kizazi chenye usawa, Angela Kairuki (katikati), akizungumza na wajumbe wa Baraza la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, jijini Arusha jana. Kushoto ni Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma na Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Sauda Msemo. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Wajumbe ESARBICA wakutana kujadili utunzaji nyaraka kidijitali

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAJUMBE wa Bodi ya Wanachama wa Baraza la Nyaraka Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESARBICA), kutoka mataifa 14 wamekutana jijini Arusha kwa ajili ya kujadiliana namna ya kutunza kumbukumbu na nyaraka kwa kutumia njia za kidijitali.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Xavier Daudi, wakati akifungua Mkutano wa 59 wa ESARBICA.

Alisema Serikali ya Tanzania imepiga hatua katika utumiaji mfumo wa kidijitali kwa kuwa mashirika na taasisi za umma zimefikia asilimia 50 wa utumiaji wa teknolojia hiyo.

Alisema awali kwa asili ya utunzaji wa nyaraka walikuwa wakitumia kuhifadhi kwa mfumo wa makaratasi, lakini kutokana na kukua kwa teknolojia wanasisitiza utumiaji wa njia za kidijitali.

Alisema nyaraka na kumbukumbu ni moyo wa serikali kwa sababu unapokuwa na kumbukumbu sahihi za kidijitali inasaidia kuongeza ufanisi wa kazi kwa serikali.

"Tunasisitiza kutumia teknolojia japokuwa kuna baadhi ya changamoto ikiwamo ya wataalamu lakini wanajitahidi sana kuzima majaribio ambayo ni hatarishi yanayoweza kusababisha tusifanikiwe kwenye dhamira," alisema.

Licha ya kuzungumza hayo, alizitaka taasisi za nchi wanachama wa baraza hilo kutumia mifumo ya kisasa kwa kuwa itasaidia kuleta mabadiliko kwa kasi zaidi.

"Tunaelekea huko tutahakikisha kuwa mifumo yote ya serikali inazungumza ili mwananchi apate huduma bila ya kufika kwenye ofisi za umma," alisema.

Aidha, alisema hivi karibuni huko Korea Kusini nchi ya Tanzania ilipatiwa tuzo kutoka Umoja wa Mataifa (UN), kwa kuwa na mfumo bora uliobuniwa na serikali wa E-mrejesho.

Rais wa ESARBICA, Pulenga Kekana, alisema mkutano huo utafanyika kwa siku tatu kuanzia Agosti 19 hadi 20,2024 na wajumbe wametoka katika nchi 14 wanachama wa umoja huo.

Naye Mkurugenzi Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Firimin Msiangi, alisema kazi ya bodi hiyo ni kubadilishana uzoefu na kujadiliana mambo mbalimbali ikiwamo kuhakikisha sekta hiyo inaboreshwa.



# Maabara zatibua bei ya almasi duniani

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

BEI ya almasi imeshuka duniani kwa kile kinachodaiwa ni maabara za uzalishaji wa madini hayo kuuza kwa bei ya chini.

Madai hayo yalitolewa juzi na Meneja Mkuu wa Mgodi wa Almasi Mwadui (WDL) uliopo wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga, Ayoub Mwenda wakati akitoa taarifa kwa Waziri wa Madini, Anthony Mavunde alipotembelea mgodi huo.

Mwenda alisema licha ya uzalishaji wa almasi kuongezeka katika mgodi huo, lakini umeathiriwa na maabara hizo kwa kuuza madini hayo kwa kushusha bei.

Alisema hali hiyo imesababisha kuanza kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na watoa huduma ndani ya mgodi huo.

"Mikakati tuliyonayo ili kukabiliana na soko hilo ni kuongeza ukubwa wa almasi na kuiongezea thamani na ubora zaidi ili kuzizidi almasi za kwenye maabara," alisema Mwenda.

Waziri Mavunde, alisema tatizo la kushuka kwa soko la almasi ni la dunia nzima na siyo Mwadui pekee.

Alisema Serikali itaendelea kushirikiana na mgodi huo kutatua tatizo hilo na kurudisha hadhi ya madini hayo.

Aliuagiza mgodi huo kukutana na watoa huduma ndani ya mgodi huo na kuwaeleza hali halisi ya kushuka kwa soko hilo badala ya kuchukua uamuzi wa kupunguza bila kuwapatia taarifa ili wajipange.




Mshindi wa kampeni ya Shinda Mechi Zako Kinamna yako ya Benki ya NBC, inayolenga kuchochea ukuaji wa uchumi miongoni mwa wateja wake kupitia uwekaji wa akiba, Renalda Lema (kushoto), akipokea zawadi ya friji mpya kutoka kwa Meneja wa Benki hiyo, Tawi la Mbezi Beach, Pudensiana Lihamwike, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanawake, vijana, wenye ulemavu wajengewa jengo la mikopo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Ushetu iliyopo Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga inatarajia kutumia zaidi ya Sh.milioni 47.1 kujenga jengo litakalotumika kutoa mikopo ya silimia 10 kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Akitoa taarifa ujenzi wa jengo hilo mbele ya Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu, Godfrey Mnzava, Ofisa Maendeleo ya Jamii, wa Halmashauri hiyo, Fabiano Abisai, alisema kati ya fedha hizo, Sh.milioni 31.6 zimetokana na mapato ya ndani ya halmashauri.

Abisai, alizitaja ofisi nyingine zitakazojengwa katika jengo hilo kuwa ni ya uongozi wa wamachinga, bodaboda, katibu muhtasi na ukumbi wa mikutano.

Alisema wazo la ujenzi huo lilitokana na umuhimu wa kundi hilo katika kuchangia uchumi wa mtu mmoja mmoja, familia, halmashauri na Taifa.

"Halmashauri imetenga Sh.milioni 15 kukamilisha mradi huu na pia wananchi wamechangia ujenzi kwa Sh.568,000," alisema Abisai.

Akizungumza baada ya kupokea taarifa hiyo, Mnzava aliipongeza halmashauri hiyo kwa kubuni mradi huo wa kuratibu shughuli za kutoa mikopo na kurejesha kwa makundi hayo.

Aliwataka walengwa hao kuwa wazalendo kwa kuzitumia ofisi hizo kwa malengo yaliyokusudiwa badala ya kugeuza vijiwe vya kutumia dawa za kulevya hususani bangi na mirungi.

Kwa upande mwingine, alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kuendelea kupambana na matumizi ya dawa hizo kwa vijana na kuwataka askari wake kuendelea kufanya doria na ukaguzi ili kudhibiti kutapakaa mitaani.

## Wakulima wahimizwa kutumia mbolea

**Na Renatha Msungu,** KAGERA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Fatma Mwassa amehimiza matumizi bora ya mbolea kwa wakulima ili wapate mavuno mengi na kukuza uchumi wao.

Mwassa alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa ufunguzi wa kampeni ya 'Kilimo ni Mbolea' iliyolenga kuelimisha umma kuhusu matumizi sahihi ya mbolea na kuhamasisha usajili wa wakulima kwenye mfumo wa mbolea ya ruzuku.

Aliwataka wakulima kujitokeza kujisajili kwenye mfumo huo ili waweze kununua mbolea kwa bei nafuu na kuachana na kilimo cha mazoea kwa kutumia teknolojia mbalimbali ikiwemo matumizi sahihi ya mbolea.

Vilevile aliwataka maofisa ugani wa kila halmashauri mkoani hapa kutumia vizuri vifaa vya kupima udongo vilivyotolewa na Serikali ili kuwawezesha wakulima kutumia mbolea kulingana na udongo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dk. Anthony Diallo, alisema mkulima anayetumia mbolea anavuna mara 10 zaidi ya mazao kwa kuwa anaweza kulima eneo dogo na kuvuna zaidi.

# Wapewa mbinu kuongeza uzalishaji tumbaku

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WAKULIMA wa tumbaku mkoani hapa, wametakiwa kuzingatia matumizi sahihi ya mbolea wakati wa msimu mpya wa kilimo ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Ugani, Michael Zakari wakati wa mafunzo kwa wakulima na waandishi wa habari waliotembelea shamba darasa la Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku Tabora (WETCU).

Zakari, alisema kwa msimu huu wa kilimo WETCU kina vyama vya msingi (AMCOS), 252 ambavyo vinajishughulisha na kilimo cha zao hilo katika maeneo yao.

Alisisitiza kuwa wakulima hao wanatakiwa kuweka mkazo katika kilimo cha zao hilo kuzingatia taratibu za kitaalamu katika kulitunza.

Mjumbe wa Bodi ya WETCU, Abdallah Iddi, alisema chama hicho kimeanzisha utaratibu wa kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kupitia shamba darasa ili kuwasaidia kufikia malengo yao.

Mjumbe wa Bodi hiyo kutoka Wilaya ya Nzega, Joyce Mambada alitoa wito kwa wakulima wanaopata elimu hiyo kuwa mabalozi wazuri kwa wenzao ili kuhakikisha kila mmoja anakuwa na uelewa wa matumizi sahihi ya mbolea.

Mmoja wa wakulima hao, Msanizi Abel kutoka Kata ya Igalula wilayani Uyui, aliwashukuru viongozi wa WETCU kwa kutoa elimu kwa wakulima kwa lengo la kuwasaidia kufikia malengo yao.



Ukurasa 12

**Bomboko aainisha la kufanya ili kufikia jamii yenye maadili**



Ukurasa 13

**Sera inapotajwa kuwa kikwazo marekebisho Sheria ya Habari**


# siasa

JUMATANO AGOSTI 21, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


## MSICHANA INITIATIVE:

# Inataka jibu serikali inakwama wapi hukumu Sheria ya Ndoa

- Yaligusa Bunge ni mdau lichagize kasi marekebisho

**Na Elizabeth Zaya**

BAA la umaskini linawaweka wasichana wengi wa maeneo ya jamii zisizojua umuhimu wa elimu kwenye unyanyasaji wa kijinsia ukiwamo kuozwa wakiwa wadogo na mimba za utotoni.

Hizi ni zile ndoa ambazo msichana anatolewa popote hata darasani na kuozwa hata akiwa chini ya miaka 15. Lakini, kwanini hali hii iendelee?

Shirika la Kijamii la Msichana Initiative, limeguswa na unyanyasaji huu unaoendelea likieleza kusikitishwa na kukwama mchakato wa kuifanyia mabadiliko ya vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inayoruhusu mtoto wa miaka 14 kuolewa.

Watetezi hao wa haki za wanawake na watoto wanasema ugumu uko wapi wakati vilibatilishwa na mahakama na kukumbusha kuwa licha ya kushinda kesi mara mbili mwaka 2016 na 2019 na kuamriwa kufanywa mabadiliko ya Sheria ya Ndoa, hakuna kilichofanyika.

Lucy Gidamis ni Ofisa Mwandamizi uchechemuzi wa shirika hilo, anayesema hata walipofuatilia mahakamani na kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, walijibiwa kuwa walifanya kwa sehemu yao kisheria, kazi iliyobaki inapaswa kufanywa na mamlaka nyingine.

"Tunajivunia kama shirika kutumia jukwaa letu kuhamasisha mabadiliko ya sheria iliyokuwa inaruhusu mtoto wa miaka 14 kuolewa na tunaishukuru mahakama ya rufani kupitia hukumu ambayo ilibatilisha vifungu



Mkurugenzi na Mwasisi wa Msichana Initiative, Rebeca Gyumi. **PICHA: MTANDAO**

hivyo. Kwetu sisi ni mafanikio makubwa kushinda rufani hii," anasema Lucy.

"Lakini tunachotaka kuona ni utekelezaji wa hukumu hii. Mamlaka zinazohusika likiwamo bunge, nazo zifanye kazi yake kupata mabadiliko ili kuwaweka salama watoto wa nchi hii."

Lucy anasema wanatamani kuona mchakato wa mabadiliko ya sheria ya ndoa unakamilika na unaheshimu kazi iliyofanywa na mahakama.

"Tunatamani mabadiliko ya sheria ya ndoa yakikamilika ili kuendana na maelekezo yaliyotolewa na mahakama ya rufani na kuongeza ulinzi kwa watoto wanaopitia ukatili huu," anasema Lucy.

"Wasiwasi wetu ni serikali kukaa kimya, tunaona kwamba hii itachelewesha zaidi mchakato na kufifisha umuhimu wa maelekezo yaliyotolewa na majaji wa mahakama ya rufani kuhusu sheria hii ya ndoa ya mwaka 1971."

Lucy anasema kwamba ni vema mamlaka zenye wajibu huo zikaheshimu uamuzi uliotolewa na mahakama kuvifanyia marekebisho ya sheria hiyo haraka kwa kubatilisha vifungu hivyo ili kuwaokoa watoto wa kike waathirika wakubwa na ndoa za utotoni.

"Hatuelewi kwa nini sheria hii haifanyiwi marekebisho licha ya kwamba mahakama imeshatoa hukumu mara kadhaa ikitaka ifanyiwe maboresho hasa kwenye vifungu hivyo vya 13 na 17, tunaiomba serikali na bunge imalize hili suala. Ni kwa sababu kufanya hivyo ni kuwaokoa watoto wa Tanzania," anasema Lucy.

Kwa mujibu wa Lucy asilimia kubwa ya watoto wanaoumia zaidi kutokana na kuwapo kwa sheria hiyo ni wale wanaotoka kwenye familia zenye umaskini ambazo huwatumia ili kujipatia kipato.

"Huwezi kusikia mtoto wa 'kigogo' anaozwa na miaka 14, ni wale wa Watanzania maskini ndiyo wanaonewa, wakati wao wanaozwa mabinti wa wakubwa wanaendelea na masomo, ifike mahali tuwaonee huruma maana nao ni watoto kama ilivyo kwa wengine, tuwalinde ili na wao watimize ndoto zao," anasema Lucy.

Dk.Avemaria Semakafu, ni Mjumbe wa Jukwaa la Wanawake Katika Uongozi, Katiba na Uchaguzi, anasema haoni sababu za kuendelea kuchelewesha mabadiliko ya sheria hiyo wakati mahakama ilishatoa hukumu ya kutaka mabadiliko yafanyike.

Anasema yapo madhara mengi yanayowapata watoto wanapoolewa katika umri mdogo, hivyo mabadiliko ya sheria hiyo ni muhimu kuimarisha ulinzi wao.

"Si tu kuimarisha ulinzi lakini endapo kutafanyika mabadiliko, itawaweka katika nafasi nzuri ya kutimiza ndoto zao kwa sababu tumeshuhudia mara kadhaa baadhi yao wakiozwa kwa nguvu na kukatisha masomo," anasema Dk.Avemaria.

Mkurugenzi wa Msichana Initiative, Rebecca Gyumi, lilifungua kesi Mahakama Kuu ya Tanzania kwa niaba ya watoto wote walio katika hatari ya kuingia kwenye ndoa za utotoni mwaka 2016 kupinga uhalali wa kikatiba wa ndoa za utotoni.

Rebecca alishinda shauri baada ya mahakama kutamka kwamba vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ni vya kibaguzi na vinakwenda kinyume cha katiba na kwamba vimepitwa na wakati.

Rebecca anapinga vifungu hivyo vya 13 na 17 kwa misingi kwamba vinakiuka ibara ya 12(1) ya Katiba ya Tanzania inayotoa usawa kwa watu wote mbele ya sheria.

Pia, alipinga kwamba vifungu hivyo vinakiuka ibara ya 13(1) (2) ya katiba hiyo ya nchi ambayo inawalinda watu dhidi ya ubaguzi kwa misingi ya kijinsia, ambayo kadhalika inaeleza kwamba watu wenye umri chini ya miaka 18 ni watoto na hawana uwezo wa kufanya uamuzi sahihi juu kuoa au kuolewa.

Kadhalika anasema kuwa vinakiuka ibara ya 21(2) ya katiba kwa kutowapa wasichana fursa ya kushiriki kikamilifu katika kuamua mustakabali wa maisha yao na kwamba vinamnyima mtoto haki ya kupata elimu na uhuru wa mawazo.

Katika shauri hilo Mahakama

INAENDELEA UK. 12

# Bomboko aainisha la kufanya ili kufikia jamii yenye maadili



Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hassan Bomboko, akizungumza kwenye moja ya majukumu yake. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wana mengi ya kujadili yanayohusu kuporomoka kwa maadili, kuanzia nchi kuwa na idadi kubwa ya wanawake na vijana wasiopenda ndoa, ndoa za jinsia moja na unyanyasaji watoto kingono.

Si hayo pekee, kuna mengine kama vijana kutumbukia kwenye ulevi kupindukia na wengi kutekwa na tabia pamoja na mitindo ya kimagharibi ambayo ni mwanzo wa mmomonyoko wa maadili.

Mijadala hiyo inapofanyika swali linakuja ni nani wa kulaumiwa kutokana na hali hiyo?

Majibu ni mengi lakini mojawapo ni watu kupendelea zaidi mila na tamaduni za Kizungu au za kimagharibi, jambo linalosababisha watu kuacha mila na desturi zao na kuingia kwenye usasa.

Kujidai kuwa wako kiteknolojia, kidijitali ndiko kunakowasumbua ikielezwa kuwa ni chanzo cha kudorora kwa maadili na kupotoka kwa watu wengi.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo jijini Dar es Salaam, Hassan Bomboko, anazitaka taasisi zisizo za kiserikali (NGOs) kuhimiza na kuheshimu mila na desturi za Mtanzania na kuacha kushangilia mila za kimagharibi, ili kupunguza mmomonyoko wa maadili unaotishia mienendo mema katika kila pembe ya nchi.

Akizungumza katika jukwaa la mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NAcoNGO 2024), wilayani Ubungo, linaloandaliwa na NAcoNGO Ubungo kwa kushirikiana na Kitengo cha Maendeleo ya Jamii Manispaa hiyo, anasema lazima kila asasi iweke maadili na uzalendo kuwa kipaumbele.

"Kama kila shirika lingesimamia lilichokikusudia iwe ni maadili, afya, kilimo, elimu, mazingira na haki za watoto Tanzania ingekuwa na jamii bora na leo hii tusingekuwa na wasichana wanaojiuza mitaani (madada poa) wala ndoa za jinsia moja."

Mkuu wa Wilaya anasema nchi inahitaji wa kuiokoa, kuilinda isiende mrama akiyataka mashirika yasiyo ya kiserikali kusimama yasiwe na woga wala kujiweka nyuma kwa kuwa yapo kwa mujibu wa sheria na ni tegemeo kubwa la serikali kusaidia kuondoa ukosefu wa maadili unaotisha.

Anawaambia washiriki kuwa serikali peke yake haiwezi inahitaji washirika kama ilivyo AZAKI na sasa zibebe jukumu la kuhamasisha uzalendo, kuacha usasa au umagharibi na kuhimiza mila na desturi za Mtanzania kuwa jambo muhimu.

"Ninyi mna haki ya kutoa matamko bila ya kuegemea upande wowote ili mradi hamvunji sheria zilizowekwa na pia kile mnachozungumza hakikisheni hakiharibu mila na desturi za nchi yetu," anasema Bomboko. Kwa mujibu wa Bomboko jamii imeacha kufuata mila na tamaduni zake na kufuata mambo ya kimagharibi mfano kwenye mavazi, mavazi vijana wanavaa ovyo, watoto hawakanywi wala kuadhibiwa, ulevi kupindukia, ngono za utotoni, ndoa za jinsia moja, uhalifu kama kutumia dawa za kulevya yote hayo akisema ni sababu zinazochangia kuwa na matatizo ya mmomonyoko wa maadili.

Anakumbusha kuwa zamani vijana na jamii ilivalia nguo za heshima muda wote. Lakini leo unapotembea barabarani ni kawaida kuona mabinti wakitembea nusu uchi na wavulana wanavaa suruali sio kiunoni.

Aidha, vijana wanajichubua ngozi, kuvuta sigara, wengine bangi na mengine ambayo yanaonyesha kuwa maadili yanatoweka kwa kasi.

Anawaahidi kuwa serikali itaendelea kushirikiana na taasisi hizo katika nyanja zote na kwamba changamoto zao zitaendelea kusikilizwa na kutatuliwa moja baada ya jingine kulingana na uwezo uliopo.

Kaulimbiu ya jukwaa hilo mwaka huu ni "Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni Wadau muhimu, Washirikishwe Kuimarisha Utawala Bora".

Jukwaa hilo likishirikisha pia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ubungo, inaonya kuhusu kugeuza fedha za AZAKI kuwa mali binafsi au za wachache.

TAKUKURU Wilaya ya Ubungo inawakumbusha viongozi wa mashirika yasiyo ya kiserikali kuepuka rushwa kwa kubadilisha matumizi ya fedha za mradi kwa manufaa ya watu binafsi na sio jamii kama mipango na mikakati inavyoeleza.

Aidha, katika jukwaa hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya kiraia ya Society Empowerment Organ (SEO), Upendo Mwinchande, akishiriki mkutano huo, anazungumzia suala la maadili akisema ili kuzuia mmomonyoko usiendelee kuumiza jamii, kila mmoja azingatie kulinda heshima.

Anasema kila mmoja asimame katika nafasi yake na awe na heshima kwa kile anachokifanya.

"Tuzingatie heshima na mwenendo mwema katika kila tunachofanya. Mfano nyumbani, kazini iwe umejiajiri au umejiriwa. Kwenye malezi, majukwaani na ndani ya nyumba za ibada tufanye kazi na majukumu yetu kwa kuzingatia heshima." Anasema Upendo.

Anaongeza kuwa maadili katika jamii yatapatikana na kuendelezwa iwapo kila mmoja au kundi litafuata, kuzingatia na kuheshimu kazi na wajibu wake bila kuiga au kupotosha ukweli na kuwajibika kulinda utu, heshima, haki, sheria na taratibu zinazoongoza jamii.

Anasema ikiwa kila mmoja atatimiza wajibu kwa haki na kuweka heshima mbele ni wazi hakutakuwa na masuala ya rushwa, rushwa za ngono, ufisadi, mimba za utotoni, ulawiti, ubakaji, unyanyasaji wa kijinsia, wa watoto wala ndoa za jinsia moja.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa ya Ubungo, Mercy Ndekeno, akizungumza kwenye kongamano hilo, anamwambia Mkuu wa Wilaya kuwa Ubungo ina AZAKI 127, zinazoshiriki katika masuala mbalimbali ya kijamii kama elimu, uhamasishaji, afya, elimu kwa vijana na ujasiriamali.

## INATAKA JIBU SERIKALI INAKWAMA WAPI HUKUMU SHERIA YA NDOA

**INATOKA UK. 11**

Kuu Julai 8, 2016, ilitoa hukumu kuwa, ndoa yoyote ya mtu mwenye umri chini ya miaka 18 ni kinyume cha sheria na kwamba vifungu hivyo vinaruhusu watoto kuingia kwenye ndoa wakati haifai kuwaingiza.

Watoto katika majukumu makubwa ya ndoa na kuonyesha hatari zake kiafya inayowakabili watoto hao pale wanapoolewa wakiwa na umri mdogo.

Mahakama ilitoa uamuzi kwamba vifungu hivyo havitoi usawa kwa msichana na mvulana katika njia mbili, kwanza umri wa ndoa tofauti kati yao, pili, wasichana chini ya umri wa miaka 18 wanahitaji ridhaa ya wazazi kuolewa wakati wavulana hawahitaji.

Inaonyesha kwamba tofauti hiyo inatoa maana kwamba wasichana na wavulana hawatendewi sawa chini ya vifungu vya 13 na 17 vya sheria ya ndoa na kuna ubaguzi na vinakiuka ibara ya 12 na 13 za katiba ya nchi.

Hata hivyo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ilikata rufani kupitia shauri namba 204 la mwaka 2017 kupinga uamuzi huo wa Mahakama Kuu lakini mwaka 2019 Mahakama ya Rufani ilimpatia tena ushindi Rebeca na kutoa mwaka mmoja sheria hiyo iwe imefanyiwa marekebisho.

Ndoa za utotoni husababisha athari mbaya za kiafya, kiuchumi na kijamii huku takwimu zikionyesha kuwa mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa asilimia 59 ya ndoa za utotoni ukifuatiwa na Tabora (58), Mara (55), Dodoma (51) na Lindi (48).

# Sera inapotajwa kuwa kikwazo marekebisho Sheria ya Habari

Na Jane Shusha

SEKTA ya habari Tanzania imeshuhudia makuzi na mapinduzi makubwa kwa miaka ya hivi karibuni yanayochangiwa na matumizi ya teknolojia.

Kutokana na mapinduzi haya, ni muhimu kuwa na sheria rafiki ambazo kuwa na uhuru wa wanahabari, vyombo na tasnia nzima kwa manufaa ya taifa.

Lakini, hali si hivyo kwa Tanzania kutokana na kubinywa kwa uhuru wa vyombo vya habari na wanahabari, ukitajwa kuwa ni moja ya changamoto kubwa kwa mujibu wa waandishi wengi.

Utafiti wa Sauti za Waandishi unaofanywa na taasisi ya kiraia TWAWEZA kwa kushirikiana na wadau wengine wa habari, asilimia 62-68 ya waandishi wanatoa taarifa kwamba vyombo vya habari haviko huru.

Wanasema havina uhuru wa kuripoti na kutoa maoni bila kudhibitiwa au kuingiliwa na wamiliki wa vyombo hivyo, serikali, watu wenye mamlaka na kampuni binafsi.

Kwa mwenye mapenzi na demokrasia anafahamu kwamba uhuru wa vyombo vya habari ni muhimili wa ustawi wa taifa lolote lile.

Ninachojiuliza ni hiki, kama waandishi wa habari hawajioni kuwa wako huru kufanya kazi zao bila kudhibitiwa, wanawezaje kuhabarisha umma ili ufanye maamuzi ukiwa na taarifa sahihi za mustakabali wa maisha na taifa lao?

Sheria zinatungwa ili kuhakikisha sekta ya habari inalindwa na haki ya uhuru wa kujieleza inatimizwa kama inavyotajwa na ibara ya 18 ya katiba ya Tanzania?

Kuna sheria mbalimbali zimetungwa kusimamia sekta hiyo mojawapo ni Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 iliyorekebishwa mwaka 2023. Sheria hii ilikuwa na malengo ya kukuza na kuilinda taaluma ya habari, lengo hili lilikaribishwa na wadau wengi wa sekta ya habari, wakiwamo wanahabari na vyombo pia.

Pamoja na malengo haya, sheria hiyo imeonekana kuwa na vikwazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na vifungu mbalimbali kudhuru uhuru wa vyombo vya habari na wanahabari kufanya kazi kwa uhuru na weledi. Ernest Sungura, Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), akizungumza katika Kongamano la Maendeleo ya Sekta Habari, anasema ili Tanzania ifikie uhuru kamili wa vyombo vya habari ni lazima kufanyike marekebisho.

Anasema yafanywe kwenye vifungu 12 vya Sheria ya Huduma za Habari ya 2016 ambavyo waandishi wa habari wamekuwa wakivilalamikia kila wakati.

"Ni imani ya wahariri na waandishi kuwa Tanzania itapaa zaidi katika viwango vya uhuru wa vyombo vya habari miaka ijayo vifungu 12, ambavyo wadau wanavilalamikia, vitafanyiwa marekebisho katika Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016," anasema Sungura. Baadhi ya vifungu ni cha 7 (2) (b) (iv) kinachotoa maelekezo kwa vyombo vya habari binafsi kuchapisha



Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari, Ernest Sungura. **PICHA: MCT**

> Kuna sheria mbalimbali zimetungwa kusimamia sekta hiyo mojawapo ni Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 iliyorekebishwa mwaka 2023. Sheria hii ilikuwa na malengo ya kukuza na kuilinda taaluma ya habari, lengo hili lilikaribishwa na wadau wengi wa sekta ya habari, wakiwamo wanahabari na vyombo pia.

habari zenye umuhimu kwa taifa kwa maelekezo ya serikali.

Tunajiuliza mhariri anawezaje kuwa na uhuru ikiwa anafanya kazi kutokana na maelezo ya serikali na si kwa kuongozwa na weledi na misingi ya kitaaluma iliyowekwa kwa manufaa ya umma?

Changamoto nyingine katika sheria ya sasa ni kwamba taarifa ambayo ni ya kweli inaweza kuchukuliwa kama kashfa, pamoja na ile ambayo ni maoni ya kweli ya mtu.

Kashfa ni jinai kwa mujibu wa sheria hii ambayo ni kinyume na viwango vya kimataifa ambapo kashfa si kosa la jinai bali madai ya kawaida.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, inatambua kuwapo malalamiko haya lakini moja ya sababu kubwa inayotolewa ni kuwa vifungu hivyo haviwezi kurekebishwa mpaka Sera ya Habari na Utangazaji Habari 2003 itakapofanyiwa marekebisho.

Kwa mfano suala la umiliki wa hisa zaidi ya asilimia 49 kwa wageni ili kuboresha uchumi wa sekta ya habari kutokana na uchumi wake kudorora kuwa na mkwamo wa kisera.

Hoja ya mgawo wa shea za umiliki wa vyombo vya habari ni hoja ndani ya Sera ya Habari.

Wizara inaona kuwa inawezekana kwa mazingira ya wakati huo wa kuanzisha sera serikali

> Changamoto nyingine katika sheria ya sasa ni kwamba taarifa ambayo ni ya kweli inaweza kuchukuliwa kama kashfa, pamoja na ile ambayo ni maoni ya kweli ya mtu.

ilisukumwa pengine kuona iwasaidie wazawa ndiyo maana zikawapo asilimia hizo.

Kinachohojiwa ni hiki sera ni kubwa kuliko sheria na kuliko kanuni.

Inawezekana ni kweli jambo la hisa za umiliki linahitaji kusubiri mabadiliko ya sera ambayo yameanza kuzungumziwa kwa kipindi kirefu.

Lakini, inakuwaje sababu ya kutofanyiwa marekebisho vifungu hivi 12 vinavyolalamikiwa visubiri marekebisho ya sera? Ni marekebisho mengi ya sheria mbalimbali yameshafanywa kwa kufuata sera iliyopo.

Swali ni kwamba marekebisho ya vifungu hivyo 12 yana tofauti ipi na ya vifungu vingine ambavyo vimeshafanyiwa marekebisho kwa sera ya sasa ya 2003?


Pamoja na hayo Waziri wa Habari alisema kuna mpango wa kupeleka mswada bungeni kubadilisha Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kuwa shirika la utangazaji la umma.

Muswada huo unapelekwa wakati mabadiliko ya sera au tangazo la serikali halijafanyiwa marekebisho ni swali ambalo wana habari wanajiuza?

Marekebisho ya sheria ni muhimu ili Tanzania kuwa na vyombo vya habari vinavyofanyakazi kwa uhuru na kutoa mchango wao kwenye ujenzi wa demokrasia imara na kufikia maendeleo endelevu.

VITA URUSI VS UKRAINE

# Mashambulizi yanapowageukia Warusi, wapinzani wadai kuteka vijiji, miji 92



Rais wa Urusi, Vladimir Putin



Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky. **PICHA: MTANDAO**

**Na Enock Charles**

NI miaka miwili na nusu sasa tangu kuanza vita vya Urusi na Ukraine, Warusi wakijiona wanawadhibiti Waukraine, leo hali si shwari kwa upande wa Urusi baada ya wapinzani wake kuingia ndani ya ardhi yake na kuisambaratisha kwa kiwango kikubwa.

Hapo awali hakuna aliyedhani kwamba siku moja taifa hilo dogo kwa eneo, uwezo wa kisiasa, kiuchumi na kijeshi lingeweza kuwa na nguvu ya kuivamia nchi kubwa kama Urusi na kuichakaza, lakini hali ndivyo ilivyo kwa sasa.

Ni takriban wiki mbili sasa tangu wanajeshi wake kuingia katika Jimbo la Kursk iliyopo Urusi huku wapiganaji wa Kirusi wakishindwa kuwaondoa wavamizi hao katika ardhi yao, jambo linalotafsiriwa kuwa ama uwezo wa kijeshi wa Urusi umepungua au Jeshi la Ukraine limeimarika tofauti na hapo awali.

Pamoja na ukweli kwamba Ukraine inapata msaada wa silaha na teknolojia kutoka mataifa ya Ulaya na Marekani lakini silaha pekee bila serikali imara na mbinu binafsi za kivita pengine mafanikio hayo yasingalikuwapo.

Rais Volodymyr Zelensky wa Ukraine, katika taarifa yake anasema lengo la uvamizi huo ni kuanzisha eneo la amani kwenye ardhi ya Urusi na itakuwa ni sehemu ya mkakati wa ulinzi kwa Ukraine kwa kuzuia mashambulizi kutokea upande wa Urusi kwenda Ukraine.

Akizungumza Jumapili iliyopita anawasifu wanajeshi wake kwa kufanya mashambulizi jimboni Kursk, akisema wamepata mafanikio makubwa ya kuharibu vifaa vya kijeshi vya Urusi.

Wakati hayo yakiendelea Rais wa Urusi, Vladimir Putin ameizuru nchi jirani ya Azerbaijan, akisaka kuungwa mkono.

Taarifa kutoka nchini humo zinasema ziara ya Putin ingechukua siku mbili na ingemalizika juzi Agosti 19. Putin anawasili katika taifa hilo wakati moto unawaka nyumbani kwake mapigano dhidi ya Jeshi la Ukraine katika mkoa wa Kursk.

Ikulu ya Urusi au Kremlin inasema ziara hiyo inalenga kuendeleza uhusiano wa ushirika wa kimkakati kati ya Azerbaijan na Urusi. Putin pia alitarajiwa kujadili mchakato wa amani kati ya Azerbaijan na Armenia na Rais Ilham Aliyev.

Wakati hali ikiwa hivyo, mshirika mwingine wa karibu wa Putin, Rais wa Beralus Alexander Lukashenko, ametangaza kupeleka theluthi ya vikosi mpakani mwa Ukraine ikiwa ni baada ya wanajeshi wa Ukraine kuvuka mpaka kwa kile alichodai anga lake limeingiliwa.

Waziri wa Ulinzi wa Belarus, Viktor Khrenin, anasema Ijumaa iliyopita kuwa kuna uwezekano mkubwa wa uchochezi wa kutumia silaha kutoka jirani yake Ukraine na kwamba hali katika eneo hilo la mpaka ni ya mvutano.

Lukashenko anaongeza kuwa mpaka wa Belarus na Ukraine unazidi kubinywa kuliko kawaida na kwamba wanajeshi wa Ukraine watapata hasara ikiwa watajaribu kuuvuka mpaka huo.

Hata hivyo, inadaiwa kuwa hakuna mshirika yeyote wa Putin anayethubutu kuingia vitani kumsaidia badala yake wameishia kutoa matamko ambayo hayana msaada kwa taifa hilo. Ni hivi karibuni Rais wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un, anatoa tamko la kulaani vikali kile alichoita uvamizi wa nchi za magharibi hasa Marekani kwa Urusi baada ya vikosi vya Ukraine kuvuka mpaka na kuingia Urusi.

Rais Kim Jong anadai Ukraine inaungwa mkono na Marekani na mataifa mengine ya magharibi katika kufanikisha kuingia katika ardhi ya Urusi, akikiita ni kitendo cha kigaidi.

Licha ya Urusi kushindwa moja kwa moja kuingia vitani washirika wa Putin wameshindwa kutoa michango ya kutosha ya kumsaidia mwenzao kama ilivyo kwa upande wa Ukraine.

Mashambulizi ya Ukraine Jimbo la Kursk yameendelea kwa siku 15 mfululizo sasa na moja ya malengo ni kuilazimisha Urusi kupeleka tena wanajeshi kutoka sehemu nyingine za mstari wa mbele nchini Ukraine warudi Urusi kulinda mipaka.

Kwa mujibu wa taarifa hizo baada ya kuanza kwa operesheni ya Kursk, wanajeshi wa Ukraine wameeleza kupungua kwa mapigano katika maeneo mengine mengi ya mstari wa mbele.

Mchambuzi wa masuala ya kijeshi wa Ukraine Konstantin Mashovets, anasema baada ya wanajeshi wa Ukraine kuanza mashambulizi, Urusi ilipanga wanajeshi kukabiliana nao mipakani.

Mtaalamu wa kijeshi, Kanali Mstaafu, Petr Chernik, anaiambia BBC kwamba Urusi lazima ikusanye wanajeshi wasiopungua 30,000 mpaka 40,000 ili kupata mafanikio katika jimbo la Kursk.

Idadi ya wanajeshi wa Urusi katika eneo la Kursk, mtaalamu huyo anasema, inapaswa kuwa mara nne zaidi ya askari wa Ukraine. Hilo ni kutokana na ukweli kwamba Warusi pengine watalazimika kushambulia safu za ulinzi zilizowekwa na Waukraine.

Wachambuzi wa kijeshi wanaeleza kwamba hatua ya Ukraine kuingia Urusi imeongeza morali kwa wanajeshi wake na vile vile kupunguza morali kwa Warusi waliochoshwa na mapigano yaliyodumu kwa miaka miwili na nusu tofauti na ilivyotarajiwa hapo awali.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa upande wa Urusi kuchukua eneo kubwa la Ukraine lakini sasa haitakuwa na maana iwapo Ukraine itaendelea kuchukua mikoa na kukalia ardhi ya Warusi sababu itakuwa ni kama kubadlishana maeneo huku Warusi wakitakiwa kuhamia Ukraine na Waukraine wakigawiwa ardhi Urusi.

Hata hivyo , Ukraine inasema haina nia ya kupora ardhi ya Urusi bali lengo ni kulitumia eneo hilo kama mtaji wakati wa mazungumzo ya kusitisha vita ili kupata tena mikoa yake iliyochukuliwa na Urusi katika miaka miwili ya vita ambayo ni karibu asilimia 15 la ardhi yote ya taifa hilo.

Hadi juzi Ukraine ilitangaza kushikilia vijiji na miji 92 katika jimbo la Kursk ikiwa ni kilomita za mraba 1,250 za eneo la Urusi.

“Kwa ujumla, operesheni hii imekuwa uwekezaji wetu mkubwa katika mchakato wa kuwakomboa Waukraine kutoka utumwa wa Urusi. Tumeteka maeneo mengi na wafungwa wa Urusi katika operesheni yetu ndani ya Urusi, “ anasema Rais Volodymyr Zelensky, katika mkutano wa wakuu wa ujumbe wa kidiplomasia wa Ukraine.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Kamanda Mkuu wa Majeshi ya Ukraine, Oleksandr Syrsky, alidai kuwa jeshi lake wakati huo lilidhibiti vijiji na miji 82 ya Kursk.

*BBC SWAHILI*





## OSHA yawasilisha maboresho ya kanuni katika kamati

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umewasilisha maboresho ya kanuni mbili za usalama na afya kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Maboresho hayo ambayo yamefanyika katika Kanuni za Igonomia na Mazingira ya Kazi yalishauriwa kufanywa na kamati hiyo katika kikao chake cha Oktoba 26 mwaka jana baada ya OSHA kuwasilisha kanuni hizo.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Patrobas Katambi, aliwasilisha wasilisho hilo kwa niaba ya waziri wa wizara hiyo, Ridhiwani Kikwete.

Katambi aliambatana na Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, Kamishna wa Kazi, Suzan Mkangwa na watendaji wengine wa wizara na Taasisi ya OSHA.

Katambi ameiambia kamati kuwa mapendekezo yote yaliyotolewa ikiwamo kujumuisha tafsiri ya neno mamlaka pamoja kuondoa maudhui yanayojirudia katika kanuni hizo yameshughulikiwa.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Jasson Rweikiza, aliipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) pamoja na OSHA kwa kupokea na kutekeleza maagizo ya kamati yake.

Aidha, aliahidi kamati yake kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi chini yake katika kuwahudumia wananchi kupitia ushauri na maelekezo mbalimbali yanayolenga kuboresha utendaji wa serikali.

Wakati huo huo, OSHA imekutana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na kufanya wasilisho kuhusu utendaji.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, aliieleza kamati hiyo umuhimu wa kulinda nguvu kazi ya taifa kupitia uimarishaji wa mifumo ya usalama na afya katika sehemu za kazi.

Alisema: "Tunachokifanya OSHA ni kushauri na kusimamia maeneo ya kazi kuweka mifumo madhubuti ya kuwalinda wafanyakazi dhidi ya vihatarishi vya magonjwa pamoja na kulinda mitaji ya wawekezaji, ili kuleta tija katika uzalishaji pamoja na kulinda ustawi wa wafanyakazi."

# AG asisitiza kufanya kazi kwa weledi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, amewataka watumishi wa ofisi hiyo kufanya kazi kwa weledi ili kuongeza ubora na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku ya kuwatumikia wananchi.

Alitoa wito huo juzi jijini hapa, wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya ofisi na aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Jaji, Dk. Eliezer Feleshi.

Alisema watumishi wa ofisi yake wanapaswa kufanya kazi kwa weledi ili kuongeza ubora na ufanisi katika kuwahudumia wananchi wenye changamoto mbalimbali za kisheria.

"Niwaombe watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kufanya kazi kwa kuzingatia weledi ili kuongeza ubora na ufanisi wakati wa kutekeleza majukumu yenu ya kuwahudumia Watanzania," alisema Johari.

Aidha, aliitaka menejimenti na watumishi wa ofisi yake kufanya kazi kwa bidii, huku wakiifuata na kuiishi kauli mbiu ya ofisi hiyo ya weledi na ubora.

Katika makabidhiano hayo, Johari aliambatana na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Johari alimshukuru aliyekuwa mtangulizi wake, Jaji Dk. Eliezer Feleshi, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Balozi Prof. Kennedy Gastorn, menejimenti na watumishi wa ofisi hiyo kwa mapokezo mazuri.

"Nawashukuru sana kwa mapokezi mazuri mliyonipatia kwa kifupi niwasisitizie kuwajibika kwenye majukumu yetu ili tufikie malengo yetu kwa kufuata misingi ya weledi na ubora," alisema.

Kadhalika, aliahidi ushirikiano kwa menejimenti na watumishi wa ofisi hiyo katika kufanikisha utelekezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno, akizungumza wakati wa hafla hiyo alisisitiza kufanya kazi kwa bidii ili kuyafikia malengo ya ofisi hiyo.

"Ofisi yetu hii ina majukumu makubwa na mteja wake namba moja ni serikali kwahiyo ili kufanikisha na kuifikia kauli mbiu yetu ya weledi na ubora kutatokana na ushirikiano baina yetu ninyi na sisi," alisema.

Kwa upande wake Jaji Dk. Eliezer Feleshi aliwapongeza kwa kupata uteuzi huo na kuwaahidi ushirikiano kwenye masuala mbalimbali kila itakapohitajika.

Kadhalika, aliitaka Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kuwapa ushirikiano viongozi hao.

Alisema: "Niwapongeze sana kwa kupata uteuzi huu na nina imani mtaifanya ofisi hii kuwa juu zaidi kwenye kuisaidia serikali, hapa tuna timu nzuri ya menejimenti niwaombe wajumbe wa menejimenti kuwapa ushirikiano viongozi hawa ili watekeleze majukumu yao vizuri na kwa ufanisi".



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Abbas (wa pili kushoto), akijibu hoja za Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), walipokutana Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Walimu Lulumba watakaofaulisha kupewa motisha

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Iramba mkoani Singida imeanzisha utaratibu wa kutoa motisha ya Sh. 50,000 kwa walimu katika Shule ya Sekondari Lulumba watakaofaulisha kwa ufaulu wa daraja A.

Katibu Tawala Wilaya ya Iramba, Warda Abdallah Obathany, alitangaza utaratibu huo juzi wakati wa hafla ya kutoa motisha kwa walimu waliofanya vizuri kitaaluma kwenye matokeo ya mitihani ya kitaifa ya kidato cha pili, nne na sita mwaka 2023/2024 wa shule hiyo.

Alisema utaratibu uliowekwa na uongozi wa shule hiyo wa kutoa Sh.20,000 kwa kila mwanafunzi aliyefaulisha vizuri masomo yake ni mzuri, kwamba unapaswa kuigwa na shule nyingine.

Obathany alisema kutokana na utaratibu huo kuwa mzuri ataunga mkono kwa kuongeza Sh.30,000 ili kifike kiwango cha Sh.50,000 ambazo atakuwa akipewa kila mwalimu wa shule hiyo.

"Nikupongeze Mkuu wa Shule ya Sekondari Lulumba, Jeremia Kitiku na bodi yako ya shule kwa uamuzi mzuri wa kutoa motisha kwa walimu wanaofanya wa kununua kila A kwa Sh. 20,000 kwa kidato cha nne na sita," alisema.

Mkuu wa Shule hiyo, Jeremia Kitiku alisema walimu wamejipanga kuhakikisha wanafuta ufaulu wa daraja la nne kwa kidato cha nne na ufaulu wa daraja la pili kwa kidato cha sita.

"Kwa miaka mitano mfululizo tumefanikiwa kufuta ufaulu wa daraja sifuri kwa kidato cha nne na pia kidato cha sita na tumejiwekea mikakati ya kuhakikisha tunaendelea kufanya vizuri kitaaluma," alisema.

Alisema mwaka jana walimu na wanafunzi katika shule za msingi wilayani Iramba walipewa motisha ya zawadi mbalimbali zikiwamo fedha taslimu Sh. milioni 14.5.

Alisema motisha hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, kwa walimu na wanafunzi 10 waliofaulu kwa kiwango cha juu kwenye mitihani hiyo.

Katika hafla hiyo walimu waliofaulisha katika masomo yao, shule zilizoongeza ufaulu na shule zilizoongoza kwa kata zilipewa zawadi ya kompyuta.





# Shangwe yatawala waliosomeshwa na Dk. Tulia ughaibuni wakirejea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

FURAHA, shangwe vilitawala katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) wakati wa mapokezi ya wanafunzi wanne wanaotoka katika mazingira magumu ambao wanasomeshwa nchini Nigeria na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson.

Tukio hilo lilitokea wakati wanafunzi hao wakirejea nyumbani kwa ajili ya likizo fupi baada ya kuishi Nigeria kwa miaka sita bila kuonana na ndugu zao wanaoishi katika maeneo mbalimbali nchini.

Baada ya taarifa kutolewa kwamba vijana hao wanarejea likizo, wazazi na walezi wao walipiga kambi katika Uwanja wa Ndege wa Songwe kwa ajili ya kuwapokea na baada ya vijana hao kutua viliibuka vilio vya furaha.

Vijana hao ni Anna Shitindi, Benard Fuine, Beauti Mwasolokoto, Ayubu Andrew na Suzana Mwakilima ambao wamesomeshwa na Dk. Tulia kuanzia kidato cha kwanza mpaka kidato cha sita na sasa wanatarajia kujiunga na masomo ya elimu ya juu.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Anna alisema kabla ya kupata ufadhili huo wa masomo kwa Dk. Tulia, walikuwa wamekata tamaa ya kuendelea na masomo kutokana na hali ngumu za maisha walizokuwa wanapitia.

Alisema kwa kipindi chote cha miaka sita waliyokuwa wakiishi Nigeria walikuwa wanahudumiwa na spika na hawakuwahi kuonana na ndugu zao zaidi ya kuwasiliana nao kwa njia ya simu.

Alisema Dk. Tulia amewaonesha moyo wa kipekee kupitia Taasisi ya Tulia Trust kwa maelezo kuwa, amefufua ndoto zao ambazo zilikuwa zinaelekea kufa.

"Dk. Tulia ni kiongozi wa mfano Tanzania, Afrika na duniani kwa kujitoa kwa ajili ya maisha ya watu wengine, huyu kiongozi ni kama mshumaa ambao huwa unateketea huku ukiwaangaza watu," alisema Anna.

Naye Ayub alisema yeye alifiwa na mama yake akiwa mdogo na maisha yake yote amelelewa na ndugu zake wengine ambao maisha yao ni ya chini na wasingeweza kumsaidia kusoma shule.

Alisema alikuwa anapenda shule lakini hali ya maisha ya ndugu zake ilikuwa inamfanya asiendelee na masomo mpaka alipopata ufadhili huo.

Alimshukuru kiongozi huyo kwa kuwasaidia na akamwomba aendelee kuwasaidia mpaka watakapohitimu masomo ya elimu ya juu, huku akimuomba pia kuwasaidia watoto wengine wanaotoka kwenye familia duni.

Mmoja wa wazazi wa vijana hao, Gerald Andrew ambaye ni kaka yake Ayub alisema familia yao ilikuwa haina uwezo wa kumsomesha kijana huyo kwa kiwango alichofikia.

Alisema Dk. Tulia kupitia taasisi yake amewasaidia kupeleka mwanga kwenye familia yao na hivyo akawaomba Watanzania wengine wenye uwezo kuiga mfano huo wa kusaidia watu wasiojiweza.

Meneja wa Taasisi ya Tulia Trust, Jacqueline Boaz, alisema vijana hao wamerejea kwa ajili ya likizo ya wiki moja na watarudi tena Nigeria kwa ajili ya kuendelea na masomo ya elimu ya juu baada ya kufanya vizuri mtihani wa kidato cha sita.

Alisema mbali na wanafunzi hao pia wapo wengine ambao wanasomeshwa hapa nchini kwa lengo la kuwasaidia kutimiza ndoto zao zilizokuwa zinataka kupotea kutokana na hali ngumu ya maisha.



Vijana wa kitanzania wanaosomeshwa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson nchini Nigeria (wenye fulana nyeupe), wakilakiana na ndugu zao baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) juzi, ikiwa ni miaka sita tangu walipokwenda masomoni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TUGHE: Kuna wanasiasa wanawabughudhi watumishi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWENYEKITI wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE) Mkoa wa Njombe, Dk. Mashaka Kisulila, amesema kuna malalamiko ya baadhi ya wanasiasa kuwabughudhi watumishi wa umma bila kujali ubinadamu wala utu.

Alitoa kauli hiyo juzi katika Mkutano Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya nchini TUGHE Mkoa wa Njombe uliofanyika mjini hapa.

Alisema chama kimekuwa kikipokea malalamiko ya kunyanyaswa kutoka kwa wanachama wao, jambo ambalo halipaswi kukaliwa kimya kwa sababu hali hiyo inaondoa molari ya kufanya kazi.

"Kuna matukio mengi tumepokea na ndiyo maana tunayasema hapa na sio kuyapokea tu pia tumeyaona, mtumishi mwingine anafayiwa kitu ambacho siyo sahihi na siyo utaratibu unaotakiwa anaonewa tu na wakati mwingine katika kuonewa hawazingatii hata ubinadamu," alisema Dk. Kisulila.

Hivyo, aliomba kuwepo na utaratibu wa kufanyika mazungumzo kuliko kutumia kauli za dhihaka na udhalilishaji bila kujali athari na utu wa mtumishi.

Aidha, alitoa pongeza kwa kuongezwa kwa asilimia za kikokotoo, hivyo kuwataka watumishi kufanya kazi kwa bidii ili wawe na haki ya kudai stahiki zao kwa mwajiri.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka aliwataka wanasiasa mkoani humo kufanya shughuli zao kwa weredi bila ya kubughudhi watumishi.

"Hairuhusiwi mtu yeyote hata kama ni mwanasiasa kumdhalilisha mtumishi wa umma kwa sababu hawezi kukushtaki ni jambo ambalo siyo sawa na halijakaa vizuri na endapo tutalibaini katika wilaya yetu tutalifanyia kazi," alisema Kasongwa.

Hata hivyo, aliwatahadhalisha watumishi wa umma mkoani Njombe kuwa makini na mitandao ya kijamii ili kulinda miiko na maadili ya kazi zao.

Mwenyekiti wa Kamati za Wanawake TUGHE Mkoa wa Njombe, Lilian Nyemele, alisisitiza haki na wajibu kwa watumishi wa umma kwa kufuata miongozo ya kazi.

# Viongozi wa dini watwishwa zigo vita ukatili

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

VIONGOZI wa dini nchini wametakiwa kuisaidia serikali kukemea vitendo vya ukatili dhidi ya makundi maalumu yakiwamo mauaji ya watu wenye ualbino na ubakaji dhidi ya watoto ili kuendelea kudumisha amani.

Aidha, wametakiwa kusaidia kukemea ukiukwaji wa maadili ya Kitanzania kwa vijana ili kujenga taifa lenye watu wenye maadili mema jambo ambalo litasaidia pia kuwa na viongozi bora.

Ofisa Tawala wa Wilaya ya Rungwe, Amimu Mwandelile aliyasema hayo kwenye hafla ya kuwekwa wakfu maaskofu na wachungaji wa Kanisa la Urejesho Pentekoste Tanzania (KLUPT) iliyofanyika katika Kijiji cha Isyonje, Kata ya Isongole wilayani humo.

Alisema mauaji ya watu wenye ualbino na ubakaji wa watoto vimekuwa ni miongoni mwa vitendo ambavyo vimekuwa vikilichafua taifa na hivyo akaomba kila mmoja ashiriki kukemea ili wanaotekeleza vitendo hivyo waache.

"Naomba mtusaidie sana kukemea vitendo hivi, watu wenye ualbino ni wenzetu, tofauti zilizopo ni za kisayansi tu, kwa hiyo wanaowaua wanakiuka haki za binadamu ambazo zipo kisheria," alisema Mwandelile.

Naye Askofu wa Kanisa la Free Church in Christ (FCC), Yohana Chaula, aliwataka wachungaji kusimamia maadili kwenye jamii hasa kwa kutoa mafundisho ambayo yatabadili fikra na mitazamo ya vijana.

Alisema wakati huu wa kuelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani, viongozi wa dini wanatakiwa kuliombea taifa ili lisiingie kwenye machafuko.

Alisema vijana ni kundi ambalo linatakiwa kuhubiriwa zaidi kutokana na kuwa kundi hatarishi kwa madai kuwa wapo baadhi yao wanatumia dawa za kulevya na ulevi wa kupindukia.



## Serikali yaelekeza nguvu utalii wa michezo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, amesema wameelekeza nguvu katika utalii mwingine, ukiachana na utalii wa fukwe, ambao utaweza kuvitangaza zaidi visiwa vya Zanzibar.

Aliyasema hayo juzi visiwani hapa, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mashindano ya resi za vishada baharini yaliopewa jina la 'Zanzibar CUB Kusi' yanayotarajiwa kufanyika Agosti 24 mwaka huu eneo la Kiwengwa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema utalii wa michezo ni mojawapo ya sekta inayokuwa kwa kasi katika utalii, kwamba watalii zaidi wanavutiwa zaidi na shughuli za michezo wakati wa safari zao.

"Kwa kuona fursa hii inayoweza kupatikana katika aina hii ya utalii, Kamisheni ya Utalii ikishirikiana kwa karibu sana na Baraza la Taifa la Michezo katika kuinua utalii wa michezo ambao unaenda sambamba na sera ya serikali ya uchumi wa bluu" alisema Jumbe.

Alisema Zanzibar imebarikiwa kuwa na utajiri wa kiutamaduni na historia ya urithi wa kale na ndiyo maana huvuna watalii kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Alisema utalii wa michezo ni suala mtambuka kwa maendeleo ya jamii na Uchumi, hivyo mashindano hayo ni alama ya utalii wa nchi mbalimbali.

Alisema Zanzibar inafursa ya kipekee katika kuutangaza mchezo huo katika masoko ya ndani na yakimataifa.

Alisema Zanzibar inatambulika ulimwenguni kuwa ni visiwa vya urithi wa kimataifa wa UNESCO, hivyo mchezo huo utaitangaza Zanzibar.

Alisema mashindano hayo yatapelekea kuongeza idadi ya vivutio vya utalii, kuongeza makazi ya watalii na kuongeza mapato ya nchi.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo Zanzibar, Said Marine alisema serikali imefanya ukarabati miundombinu ya michezo iliyopo lakini pia kujenga miundombinu mipya ambayo itaifanya Zanzibar kutimiza lengo lake la kuwa kitovu cha michezo katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

**Alisema Zanzibar inafursa ya kipekee katika kuutangaza mchezo huo katika masoko ya ndani na yakimataifa.**

# Serikali yachukua tahadhari ugonjwa wa homa ya nyani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imeanza kuchukua hatua ya tahadhari dhidi ya ugonjwa wa homa ya nyani, kutokana na kuripotiwa ongezeko la maambukizi katika nchi jirani ya Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Waziri wa Afya, Nasor Ahmed Mazrui, alisema wizara imeimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa magonjwa hasa katika viwanja vya ndege na bandari, kwa kuimarisha uchunguzi wa afya kwa wasafiri wanaoingia nchini.

Alisema pia imeanza kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya juu ya kutambua na kutoa huduma pamoja na kujikinga na ugonjwa huo.

Mazrui alisema wizara itatoa elimu kwa wananchi ili kuchukua hatua na kujikinga dhidi ya ugonjwa huo na kuhakikisha vifaa tiba na kinga vipo maeneo ya kutolea huduma.

Aidha, aliwataka wananchi kuhakikisha wanatoa taarifa kwa kupiga simu namba 190 bila ya malipo endapo watamuona mtu ana dalili za ugonjwa huo.

Alisema wananchi wanapaswa kuepuka kugusa majimaji ya mwili au ngozi ya mtu mwenye dalili ya ugonjwa huo pamoja na kugusana.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kumekuwa na jumla ya visa 38,465 na vifo 1,456 vimetokea nchi za Afrika kuanzia Januari mwaka 2022 hadi Julai mwaka huu.




Katibu wa Jumuiya ya Mabaharia Wanawake Zanzibar, Raya Khalfan, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, wakati wa hafla ya utiaji saini makubaliano ya ushirikiano wa kuanzisha Chuo cha Mabaharia Zanzibar kati ya Wizara ya Uchumi wa Bluu na Kampuni ya Heroes ya Uholanzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Chuo cha Mabaharia kuanzishwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi imetiliana saini ya makubaliano na kampuni ya Heroes kutoka Uholanzi ya kuwa na chuo cha Mabaharia ambacho kitatoa vyeti vya umahiri vinavyotambulika duniani.

Hatua hiyo itatatua changamoto ya Zanzibar kutokuwa na mabaharia wenye vyeti vya umahiri ambavyo vinatambulika kimataifa.

Makubaliano hayo yalisainiwa na Katibu Mkuu wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Kepteni Hamadi Bakari Hamad na Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Eric Janderoode.

Akizungumza baada ya utiaji saini, Waziri wa wizara hiyo Othman Shabani alisema kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto ya mabaharia wa Zanzibar kukosa sifa stahiki kutumika katika meli za kimataifa.

Alisema kozi ya ubaharia itakayotolewa itakuwa chini ya uongozi wa Chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na itasaidia kutatua changamoto hiyo na mabaharia kupata sifa stahiki na kuwa sawa na mabaharia wengine duniani.

Aidha, alisema mafunzo hayo yatakayotolewa yatatoa fursa kwa vijana wa Zanzibar kupata utaalamu na kupata vyeti ambavyo vitawawezesha kufanya kazi ndani na nje.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Kepteni Hamad Bakari Hamad, alisema mabaharia duniani wenye ngazi ya maofisa ni wachache na wanahitajika kwa wingi lakini Zanzibar mabaharia wake ni walio chini ya ngazi ya maofisa.

"Kuwa na mabaharia waliochini ya ngazi ya maofisa ni changamoto katika soko la dunia la ubaharia na hawawezi kuingia katika soko hilo kutokana na sifa zao zipo chini"alisema Kepteni Hamad.

Alisema mabaharia wengi duniani wanaofanya kazi katika meli kubwa za kimataifa ambao wenye sifa za ngazi za maofisa wanatoka nchini za India, Urusi na Ukraine.

Alisema chuo hicho cha ubaharia kitakuwa chini ya uongozi wa SUZA na darasa la kwanza litaanza mwaka huu na walimu, hivyo ni fursa nzuri kwa viajna wa Zanzibar kusomea kozi hiyo.

Naibu Makamu wa SUZA (Mipango, Fedha na Utawala), Dk. Hashim Habib, alisema ni faraja kubwa kuwepo kwa chuo hicho na kutokana na umuhimu wa kukuza uchumi wa buluu kumeleta faraja kwa sababu Zanzibar inatoa mabaharia wengi lakini kwa viwango vya chini.

Katibu wa Jumuiya ya Wanawake Mabaharia Zanzibar, Raya Khalfan, alisema kuwa Wazanzibar wengi wanashindwa kupata kazi katika meli za kimataifa kutokana na kutokuwa na sifa zinazohitajika.

Alisema kuwepo kwa chuo hicho kutaongeza idadi ya mabaharia wanawake ambao ni wachache ikilinganishwa na wanaume.

Aidha, alisema wanawake wanasomea fani ya ubaharia lakini hupangiwa kazi za uhudumu katika meli badala ya kupangiwa kazi ya ukpteni au injinia, jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi za wanawake katika kusomea fani hiyo.

Alisema wanawake wanaweza kufanya kazi vizuri za kuongoza meli, lakini hawapewi nafasi kutokana na mfumo dume uliopo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**MBARUKU HAMADI HAJI** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye usajili namba **MC 291 CTA, MC 612 DDH, MC 991 CME, MC 675 CSC.** Kwa yeyote atakaezionа atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/175525/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**SADATI SIRAJI RWEYEMAMU** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye usajili namba **MC 527 CZR.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA:PHQ/SHI/KAH/5672/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**EMMANUEL CHARLES LUPIA** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye usajili namba **MC 899 DNX, MC 666 DLW, MC 123 DNY na MC 191 DNY.**kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/RUK/SUM/865/2023, PHQ/RUK/SUM/864/2023**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**TANZANIA CHINA TRADE & TOURISM DEVELOPMENT LTD** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye usajili namba **MC 299 DTT, MC 731 DKT, MC 682 DGM, MC 789 DJC.**kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/RU/SUM/2847/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IZDORY MARCUS NYANGALIMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA ISUZU YENYE USAJILI **T184BSZ** RANGI NYEUPE KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/12547/2024.**

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**

**MAHALI: KIGOMA**

**MAOMBI NA 32 MWAKA 2024**

**DAUDI KIMONDO ............................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**PETER LIMBE..............................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: PETER LIMBE POPOTE ULIPO**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 10 Mwezi 10 Mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mheshimiwa F. Chinuku Mwenyekiti wa Baraza . Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 9 mwezi 8 mwaka 2024

MWENYEKITI

---

**KATIBU BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**

**ANDREA KISINGA ..........................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**BEDA BEDA TAWETE**
**EZEKIEL KILOWOKO** ............ **WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURI**

Ezekiel Kilowoko unataarifiwa kuwa Mleta Maombi amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako. Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa mdodoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zako za utetezi.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hii upande mmoja bila kujali uwepo wako.

Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 05/08/2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SONGEA

---


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Mshukiwa mauaji wanawake Kenya atoroka polisi

**NAIROBI, Kenya**

RAIA wa Kenya Collins Jumaisi aliyekiri kuhusika na mauaji ya wanawake 42 ambao baadhi miili yao ilipatikana imetupwa katika eneo la kutupa taka jijini Nairobi, ametoroka akiwa chini ya kizuizi cha polisi.

Polisi nchini humo ilibainisha hayo jana, ikieleza kwamba Jumaisi ni mshukiwa mkuu wa mauaji ya wanawake ambao miili yao ilipatikana Julai mwaka huu katika dampo kwenye eneo la Mukuru kwa Njenga, katika eneo la Embakasi, jijini Nairobi.

Pia ilielezwa kuwa mshukiwa huyo alitoroka kizuizini jana asubuhi pamoja na wafungwa wengine 12 waliokuwa katika Kituo cha Polisi cha Gigiri, jijini Nairobi,

Kwa mujibu wa ripoti ya Kurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) huko Gigiri, kutoroka kwao kuligunduliwa majira ya saa 11 alfajiri wakati wa ukaguzi wa kawaida.

Vyombo vya habari vya serikali ya Kenya vinasema miongoni mwa waliotoroka ni pamoja na raia 12 wa Eritrea ambao walikuwa wakishikiliwa kwa ukiukaji wa uhamiaji.

Ilielezwa kuwa polisi waligundua hawako wakiwaamsha washukiwa kwa chai ya asubuhi, na kwamba walikuwa wamekata matundu ya waya ambayo ni sehemu ya usalama kwa seli na kuinua ukuta wa mzunguko.

Mkurugenzi wa DCI Mohamed Amin, alithibitisha kisa hicho akisema msako mpya umeanzishwa dhidi ya mshukiwa huyo. „Inasikitisha kuwa hili limetokea lakini tunafuatilia suala hilo kwa hatua," alisema.

Aidha, ilielezwa kuwa Jumaisi alikiri kuwaua wanawake 42 lakini alikanusha mashtaka mbele ya mahakama Julai 2024, ikielezwa kuwa alikuwa amewekwa rumande akisubiri kusikilizwa kwa kesi yake Ijumaa.

Ilielezwa kuwa polisi Ijumaa iliyopita walipewa siku saba zaidi kuwazuia washukiwa watatu akiwemo Jumaisi, Amos Momanyi na Moses Ogembo wanaohusishwa na mauaji ya Kware.

Washukiwa hao walikuwa wamewasilishwa mbele ya Hakimu Mkuu wa Makadara Irine Gichobi ambako upande wa mashtaka uliitaka mahakama kuwaruhusu kuwazuia washtakiwa watatu kwa siku 21. *TRT*



Rais wa zamani wa Marekani, Barack Obama (kulia), akiwa na Makamu wa Rais na mgombea mteule katika kinyang'anyiro cha urais wa nchini humo Kamala Harris, jana. **PICHA MTANDAO.**

# WHO kusaidia nchi wanachama kukabili Mpox

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), baada ya kukutana na mkutano wa kwanza wa Kamati ya Dharura ya Kimataifa ya Kanuni za Afya kuhusu kuongezeka kwa Mpox, wamesisitiza kuwa wataendelea kuziunga mkono nchi wanachama zinazokabiliwa na maradhi hayo ikiwemo kuzisaidia kifedha na upatikanaji wa chanjo.

Kamati hiyo iliyokutana jana pia imesisitiza wasiwasi wake kuhusu kusambaa kwa Mpox, kutokana na kutokuwa na uhakika na uwezo uliopo wa kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huo katika Nchi Wanachama zinazokumbwa na milipuko.

Pia kamati ilitambua umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kuunga mkono juhudi za nchi wanachama kudhibiti kuenea kwa Mpox katika Kanda ya Afrika ya WHO ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa matumizi ya chanjo, matibabu, na uchunguzi.

"Hatua zingine ni kuhamasisha rasilimali za kifedha kwa nchi wanachama zinazokabiliwa na ongezeko la magonjwa na mipango ya harambee ya WHO na washirika, ikiwa ni pamoja na Afrika CDC," ilisema Kamati.

Hata hivyo, kamati ilionyesha kuwa uundaji wa mbinu za kimkakati kwa nchi wanachama ili kujitegemea zaidi katika kudhibiti kuenea kwa mpox ni muhimu.na kwamba maamuzi yanayotolewa yatasaidia nchi wanachama kujitolea kwa ufanisi zaidi na kuajiri rasilimali za ndani.

Kwa mujibu wa WHO) ugonjwa wa Mpox umeendelea kuenea katika nchi mbalimbali duniani. Kwa takwimu za kipindi chaJanuari 1 2022 hadi Juni 30, mwaka huu, jumla ya wagonjwa 99,176 wamethibitika kuwa na Mpox katika nchi 116 duniani ambako watu 208 sawa na asilimia 0.2 walipoteza maisha kwa sababu ya ugonjwa huo.

Kati, ya visa vyote duniani, bara la Afrika limethibitisha visa 4,232 sawa na asilimia 4.3 ya wagonjwa wote duniani. Mabara yanayoongoza kuwa na visa vingi ni Amerika ya Kaskazini na Kusini yakiwa na visa 62,904 sawa na asilimia 63.4 yakifuatiwa na Bara la Ulaya lenye visa 27,529, sawa na asilimia 27.8 ya visa vyote duniani.

Katika hatua nyingine Waziri wa Afya Jenista Mhagama, alisema nchi bado iko salama dhidi ya maradhi hayo huku akisisitiza wananchi kuendelea kuchukua tahadhari, wakati serikali ikiendelea kufanya jitihada za kuzuia Mpox kuingia nchini.

# Kenya kubinafsisha mashirika ya serikali

**NAIROBI, Kenya**

BARAZA la mawaziri la Kenya limeidhinisha muswada mpya wa ubinafsishaji ambao utawezesha nchi kubinafsisha baadhi ya mashirika ya serikali, na kwamba taifa hilo linatanguliza masoko ya mitaji kama mradi wa ukuaji wa uchumi.

Inaelezwa kuwa uamuzi wa baraza la mawaziri lililofanyika Machi 22, mwaka huu, uliidhinisha muswada mpya wa ubinafsishaji ambao utahusisha mali ya serikali kuuzwa kwa sekta binafsi kupitia masoko ya mitaji ya nchi.

Rais wa Kenya William Ruto akiwa katika hafla kwenye soko la hisa la Nairobi, alisema wataorodhesha mali zinazomilikiwa na umma hivi karibuni.

Mswada huo unapendekeza kwamba hazina ya kitaifa iunde na kuendeleza mpango wa ubinafsishaji wa serikali na kuupitisha kwa baraza la mawaziri ili kuidhinishwa, na kwamba mchakato huo hautaomba idhini ya bunge.

Ilielezwa kuwa mswada mpya ukiidhinishwa na bunge utachukua nafasi ya sheria ya ubinafsishaji ya mwaka 2005.

„Sheria iliyokuwepo hapo awali ilifanya iwe vigumu kwa Wakenya kumiliki kipande chochote cha mali ya Kenya, kukiwa na sheria mpya tunaweza kuweka demokrasia kwa utajiri wetu na kuruhusu mkenya kumiliki kipande cha kile ambacho ni cha nchi yake," alisema Rais Ruto.

Tume ya ubinafsishaji ya Kenya imetaja makampuni 25 zinazolengwa kwa ajili ya ugawaji wa fedha za serikali. Ikiwa ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Kenya, Shirika la Agrochemical and Food Corporation, Mamlaka ya Bandari ya Kenya, Kampuni ya Mafuta yani Kenya Pipeline Company na makampuni kadhaa ya sukari.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa baadhi ya wataalam wa sheria, wamekosoa kipengele cha mswada huo uliolenga kuondoa bunge katika uamuzi kuhusu ubinafsishaji, wakisema kuwa jukumu la bunge la usimamizi katika mchakato wowote ni muhimu. *TRT*

## Taifa Tenisi wenye ulemavu kwenda kujifua Afrika Kusini

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha wachezaji watano wa Timu ya Taifa ya Tanzania ya mchezo wa Tenisi kwa Watu wenye Ulemavu, kinatarajiwa kuondoka nchini Septemba 15, mwaka huu, kuelekea Afrika Kusini kuweka kambi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Afrika kwa vijana wenye umri chini ya miaka 18 yatakayoanza kutimua vumbi Septemba 19-29 nchini humo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Riziki Salum, alisema timu hiyo inaundwa na wanawake wawili pamoja na wanaume watatu.

Alisema kwa wachezaji kumi ambao watafanya vizuri katika michuano hiyo watapata nafasi ya kwenda Paris nchini Ufaransa kushiriki mashindano ya kimataifa yatakayofanyika kati ya Januari na Februari, mwakani.

Aliwataja baadhi ya wachezaji hao kuwa ni Aloyce Richard, Aida Ediger, pamoja na Esther Paul.

Alisema maandalizi yanaendelea vizuri ili kuhakikisha wanakwenda kuipeperusha vema bendera ya taifa kupitia mashindano hayo.

"Wachezaji wetu wanaendelea kufanya mazoezi kila siku katika viwanja vya Klabu ya Gymkhana, Dar es Salaam ili kuimarisha miili yao," alisema Salum.

## Nemes aitabiria Yanga makundi

**Na Shufaa Lyimo**

MLINDA mlango wa zamani wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Steven Nemes, amesema kwa namna timu ya Yanga ilivyojipanga vizuri, kuna uwezekano mkubwa wa kutinga tena hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika (CAFCL) kwa msimu huu wa 2024/2025.

Msimu uliopita Yanga ilitinga hatua hiyo kwa mara ya kwanza baada ya miaka 25, kwani kabla ya hapo mara ya mwisho kucheza hatua ya makundi ilikuwa mwaka 1998.

Hata hivyo, msimu huu imeanza tena vema hatua ya awali kwa kuifunga Vital'O ya Burundi mabao 4-0 ugenini (katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam) na sasa Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, inahitaji sare yoyote ama ushindi ili kutinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo ambayo ndiyo huamua timu zitakazofuzu makundi.

Akizungumza na Nipashe jana, kipa huyo alisema kutokana na aina ya wachezaji waliopo ndani ya kikosi hicho kila kitu kinawezekana.

"Kwa sasa naweza kusema Yanga wanafasi kubwa ya kufanya vizuri katika michezo yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika kutokana na usajili walioufanya kwa kuongeza wachezaji wenye viwango vya kimataifa," alisema Nemes.

# SIMBA QUEENS YAAHIDI KUTOA DOZI KUBWA ZAIDI CECAFA LEO

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya FAD ya Djibouti iliyopigwa Uwanja wa Abebe Bikila nchini Ethiopia juzi, kikosi cha timu ya soka ya wanawake cha Simba Queens, leo mchana kinajitupa tena, Uwanja wa Addis Ababa kucheza dhidi ya Kawempe Ladis Muslim kutoka nchini Uganda.

Kuelekea mchezo huo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Ukanda wa CECAFA, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda, alisema wanataka kushinda ikiwezekana kwa idadi kubwa ya mabao ili kufuzu hatua ya nusu fainali.

Akizungumza jana akiwa kwenye mazoezi Uwanja wa Tesfa Meda nchini humo, Mgunda alisema kulikuwa na mapungufu ambayo aliyaona katika mchezo wa juzi, hivyo alikuwa akiyarekebisha kwa ajili ya mchezo wa leo ambao utawapa uelekeo wa kusonga mbele kwenye michuano hiyo kutokea Kundi B.

"Tumepata matokeo mazuri juzi, lakini tumeshasahau, kinachofuata ni mechi nyingine, mashindano ni magumu na hakuna timu ya kubeza, kila timu hapa ni bingwa kutoka nchi iliyotoka, lakini sisi tunataka kushinda, tena kwa idadi kubwa ya mabao, ili tuweze kwenda moja kwa moja hatua ya nusu fainali," alisema Mgunda.

Kundi B lina timu nne za Simba Queens, PVP Buyenzi ya Burundi, Kawempe Muslim Ladies na FAD Djibouti, huku Kundi A likiwa na timu tano, ambazo ni CBE ya Ethiopia, Kenya Police Bullets, Yei Joint Stars na Rayon Sports Women ya Rwanda.

Bingwa wa michuano hiyo, atakata tiketi ya kufuzu fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kutoka Ukanda wa CECAFA.

Mfungaji wa ,hat-trick' katika mechi ya juzi, Asha Mwalala, alisema huo ni mwanzo tu, akiwaambia mashabiki wa Simba Queens kuwa mengi mazuri yanakuja, kwani kazi yake kubwa ni kupachika mabao ili kuipatia timu yake ushindi na mataji.

Mabao mengine ya Simba Queens, yalifungwa wachezaji wa kimataifa kutoka Kenya, Jentrix Shikangwa na Elizabeth Wambui.




Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo (katikati), akikabidhi mfano wa hundi ya udhamini wa Sh. milioni 40.5 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Usimamizi wa Michezo wa Shadaka kwa niaba ya Ndondo Cup, Shaffih Dauda (kulia). Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya SICPA, Edson Muiambo. Makabidhiano hayo yalifanyika jijini Dar es Salaam juzi wakati wa kutangaza udhamini huo. **MPIGAPICHA WETU**

# Pamba Jiji yaonya Dodoma Jiji

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Pamba Jiji, Goran Copunovic, ameionya Dodoma Jiji kuwa isitarajie mteremko katika mechi itakayocheza Jumamosi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, kwani wanataka kupata ushindi kabla ya kuondoka kwenye uwanja wao wa nyumbani kwenda kucheza dhidi ya Azam FC ugenini.

Akizungumza kutoka jijini Mwanza, kocha huyo raia wa Serbia, alisema baada ya kushindwa kuwapa mashabiki wa Pamba zawadi ya ushindi ya kupanda Ligi Kuu, sasa wanatarajia kufanya hivyo katika mchezo huo, hivyo kuionya Dodoma Jiji kuwa maumivu waliyoyapata mechi iliyopita dhidi ya Mashujaa FC yataongezwa.

"Ratiba ilivyotoka tukawa na mechi mbili za mwanzo nyumbani, moja tulicheza Ijumaa iliyopita dhidi ya Prisons, tukatoka suluhu licha ya kwa kwamba hatukucheza vibaya sana, tulitengeneza mashambulizi mazuri kipindi cha kwanza, tulikuwa na wakati mzuri sana, kipindi cha pili tulipata changamoto kidogo kwa sababu wapinzani wetu walikuwa na uzoefu mkubwa kutuzidi katika ligi.

"Ugeni wetu kwenye ligi ukasababisha tupate pointi moja, inatosha, na sasa tunajiandaa na mchezo unaofuata, tunajiandaa kwa fikra na kimawazo, tunajiamini kwa sababu tunacheza nyumbani, tunataka kushinda mechi ya kwanza baada ya kupanda Ligi Kuu, ili kuwaacha mashabiki wa Mwanza wakiwa na furaha, kabla ya kuelekea Dar es Salaam kucheza na Azam FC," alisema kocha huyo.

Pamba ambayo ilitoka suluhu dhidi ya Prisons katika mechi ya ufunguzi, itacheza dhidi ya Dodoma Jiji ambayo imetoka kufungwa bao 1-0, dhidi ya Mashujaa, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, Jumamosi iliyopita.

Baada ya mechi hiyo, itatoka kwenda jijini Dar es Salaam kuivaa Azam FC, Oktoba 21, katika mchezo wa raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RAMSDALE ATAKIWA WOLVES
KLABU ya Wolves imewasilisha pendekezo la kumsajili kipa wa England, Aaron Ramsdale kwa mkopo kutoka Arsenal na chaguo la kumnunua msimu ujao. ***(Athletic)***

### STERLING MAMBO MAGUMU
MSHAMBULIAJI wa Chelsea na England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 29, amekuwa akihojiwa na Juventus huku kukiwa na sintofahamu kuhusu mustakabali wake. ***(Mail)***

### WALKER AWANIWA AL-HILAL
KLABU ya Saudi Arabia, Al-Hilal inawataka mlinzi wa Manchester City, Kyle Walker na beki wa pembeni wa Ureno, Joao Cancelo, kwenye orodha yao ya wachezaji inaowawania. ***(Guardian)***

### GUNDOGAN ATAKIWA CITY
KLABU ya Manchester City ina nia ya kutaka kumnunua tena kiungo wa kati wa Ujerumani, Ilkay Gundogan mwenye umri wa miaka 33, kutoka Barcelona. ***(Athletic)***

### MERINO BEI ILE ILE
REAL Sociedad inakataa kupunguza thamani yao ya kumuuza kiungo wa kati wa Hispania anayelengwa na Arsenal, Mikel Merino mwenye umri wa miaka 28. (Mirror)

### TONEY ANUKIA SAUDIA
KLABU ya Brentford inamatarajio mshambuliaji wa England, Ivan Toney atajiunga na Al-Ahli katika Ligi ya Saudia na wanatumai kupokea takriban pauni milioni 50 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Times)***

### FULHAM NA ANDERSEN
KLABU ya Fulham inafikiria iwapo watarejea Crystal Palace na ofa nyingine ya kumnunua mlinzi wa Denmark, Joachim Andersen mwenye umri wa miaka 28. ***(Sky Sports)***

### FOFAFA HUYOOO MILAN
AC Milan imefikia makubaliano na Monaco kwa ajili ya kiungo wa kati wa Ufaransa, Youssouf Fofana mwenye umri wa miaka 25, ambaye pia ananyatiwa na Manchester United. ***(Mail)***

### BERGE AJADILIWA UNITED
MANCHESTER United inaendelea kujadiliana na Burnley kuhusu mkataba wa kiungo wa Norway, Sander Berge, 26. ***(Sky Sports)***

### JOHNSTON AGOMBEWA
KLABU za Stoke City, Swansea City na Oxford United vina nia ya kumsajili beki wa wa Scotland, Max Johnston mwenye umri wa miaka 20, kutoka Sturm Graz. ***(Football Insider)***

### ARCHER ANUKIA MKOPO
UNION Berlin na Getafe zinaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa England, Cameron Archer mwenye umri wa miaka 22, kwa mkopo kutoka Aston Villa. ***(Fabrizio Romano)***

### MADUEKE MIL 6
CHELSEA imeweka bei ya pauni milioni sita kwa klabu yoyote inayotaka kumsajili winga wa England, Noni Madueke, 22. ***(Athletic)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NAPOLI YAPAMBANA KUMBAKIZA OSIMHEN

**Kwa wakati huu, si sawa kusema ni hisia gani, tunafanya kazi kutafuta suluhisho bora...**

**NAPLES, Italia**

NAPOLI imeendelea kufanyia nia yao ya kumbakiza Victor Osimhen katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto, ingawa uhamisho wa mchezaji huyo anayelengwa kwa muda mrefu na Chelsea kwa sasa „umezuiwa", kulingana na mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo.

Akiwa ameifungia Napoli mabao 76 tangu alipowasili 2020, Osimhen bado hajaichezea klabu hiyo katika mechi mbili hadi sasa msimu huu kwani ana matumaini ya kuhama.

Chelsea imekuwa ikimwania Osimhen tangu msimu wa 2022, ingawa Napoli imekuwa ikidai bei ya juu kwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Nigeria.

Hivi majuzi, kumekuwa na mazungumzo ya Romelu Lukaku, ambaye bado ni mchezaji wa Chelsea, kujiunga na Napoli kama sehemu ya mkataba wa jumla ambao ungewafanya ‚The Blues' kumnasa, lakini bado Napoli wanahitaji kukohoa karibu pauni milioni 60 kwa Osimhen.

Wasiwasi wa gharama ya jumla ya dili hilo umesababisha mambo kukwama, hata hivyo, Chelsea ikitarajiwa kusubiri hadi mwisho wa dirisha la uhamisho kabla ya kujaribu kupata makubaliano juu ya mstari huo.

"Ni ukweli halisi, kile kocha Antonio Conte alisema, hali imezuiwa," alisema Giovanni Manna akiiambia Sky Sport Italia.

"Victor ni mchezaji muhimu, mwenye thamani na masharti muhimu. Nia yake iko wazi. Tulijaribu kudumisha uadilifu wa kikosi kwa wakati huu. Sisi si klabu pekee katika hali hii na tutaona kitakachotokea kwenye msimu huu. siku kumi zijazo.

"Kwa wakati huu, si sawa kusema ni hisia gani. Tunafanya kazi na wasaidizi wake kutafuta suluhisho bora. Kama tulivyosema ni mchezaji muhimu, kwa hivyo si kwamba tunaweza kumpata popote. Ana mkataba wa misimu mingine miwili, hivyo ni wazi kama hatutapata suluhu ifikapo Agosti 30, itabidi tuzungumze na mchezaji huyo."

HABARI MICHEZO

# CHELSEA WAINASA SAINI YA FELIX




**LONDON,** ENGLAND

CHELSEA imekubali makubaliano kimsingi kumsajili Joao Felix kutoka Atletico Madrid, vyanzo vimeiambia ESPN, katika hatua ambayo sasa inapaswa kumfanya Conor Gallagher kukamilisha uhamisho wake katika mwelekeo tofauti.

Mazungumzo yameongezeka katika siku za hivi majuzi huku Atletico wakihitaji kumhamisha mchezaji kabla ya kukamilisha dili la kumnunua Gallagher, ambaye amekuwa akifanya mazoezi mbali na kundi la kikosi cha kwanza.

Ada halisi haijulikani, lakini chanzo kimoja kiliiambia ESPN kifurushi cha mwisho cha Felix kinaweza kuwa na thamani ya euro milioni 50 pamoja na nyongeza.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ureno hakujumuishwa kwenye kikosi cha Diego Simeone kwa mechi yao ya kwanza ya LaLiga dhidi ya Villarreal Jumatatu.

Baada ya Atleti kutoka sare ya mabao 2-2 na Villarreal, Simeone alithibitisha kuwa kukosekana kwa Felix kulitokana na "soko la uhamisho."

"Hivi karibuni utajua nilichokwisha ambiwa," Simeone alisema huku akicheka baada ya kuulizwa kuhusu Felix.

Vyanzo vya habari vilisema kwamba Felix amekubali mkataba wa miaka sita na chaguo la miezi 12 zaidi kujiunga na klabu hiyo ambapo alikaa kwa mkopo kwa miezi sita mwaka jana, akifunga mabao manne katika mechi 20.

Gallagher sasa anatarajiwa kusafiri hadi Madrid kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 34, akiwa tayari amekubali masharti binafsi na kukamilisha uchunguzi wa afya.

Felix atakuwa mchezaji wa 11 kusajiliwa Chelsea majira haya ya kiangazi baada ya Pedro Neto, Tosin Adarabioyo, Kiernan Dewsbury-Hall, Filip Jorgensen, Omari Kellyman, Aaron Anselmino, Caleb Wiley, Renato Veiga na Marc Guiu huku Estevao Willian akikubali kujiunga na 'The Blues' mwaka 2025.

# Gundogan atangaza rasmi kustaafu soka

**BARCELONA,** HISPANIA

ILKAY Gundogan ametangaza kustaafu soka la kimataifa akiwa na Ujerumani baada ya kuwa nahodha wa taifa lake katika michuano ya nyumbani ya Ulaya mapema msimu huu wa majira ya joto.

Kiungo huyo wa kati wa Barcelona mwenye umri wa miaka 33, alifunga mabao 19 katika mechi 82 alizoichezea nchi yake. Alitangaza uamuzi wake kwenye mitandao ya kijamii.

"Baada ya wiki chache za kutafakari, nimefikia hitimisho kwamba ni wakati wa kumaliza kazi yangu ya timu ya taifa," aliandika.

"Ninatazama nyuma kwa fahari kubwa kwenye mechi 82 za kimataifa za nchi yangu - idadi ambayo sikuwahi kuitamani nilipoichezea timu ya taifa ya wakubwa mwaka 2011.

"Kielelezo changu hakika kilikuwa heshima kubwa ya kuweza kuiongoza timu kama nahodha kwenye mashindano yetu ya nyumbani ya Ulaya msimu uliopita wa majira ya joto! Baada ya miaka hii yote, hatimaye tuliweza kulifanya taifa lijivunie tena - nina furaha sana kwamba niliweza kuchukua sehemu katika hilo.

"Lakini hata kabla ya mashindano, nilihisi uchovu fulani mwilini mwangu na pia kichwani mwangu, jambo ambalo lilinifanya nifikirie. Na idadi ya michezo katika ngazi ya klabu na taifa haipungui.

"Bila shaka nitaendelea kuwa shabiki wa timu hii ya taifa na ninatumai kuwa tunaweza kuendeleza hali ya juu pamoja - na kisha hakuna kitu cha kutuzuia kuwa mmoja wa washindani wakuu wa taji kwenye Kombe la Dunia la 2026. Tuna kocha mzuri, kikosi chenye nguvu na ari ya timu."

Kustaafu kwa Gundogan kunakuja baada ya Thomas Muller, ambaye alitangaza kujiuzulu wadhifa wake wa kimataifa baada ya kampeni ya Euro 2024 ambayo ilishuhudia Ujerumani ikitolewa na Hispania katika robo fainali.

# Roque kuondoka Barcelona

**BARCELONA,** HISPANIA

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Vitor Roque, anaonekana kana kwamba atalazimika kuhama klabu hiyo katika kipindi kilichosalia cha dirisha la usajili la majira haya ya joto.

Roque aliwasili kutoka Athletico Paranaense Januari kwa mkataba ulioanza kwa euro milioni 30 na thamani yake ilikuwa euro milioni 61 na nyongeza.

Lakini alipewa dakika 353 tu katika mechi 16. Mustakabali wake umekuwa shakani tangu mwishoni mwa msimu uliopita na hajaimarika kutokana na mabadiliko ya kocha.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, hakuonekana wakati Barcelona ikifungua kampeni yake mpya ya LaLiga kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Valencia Jumamosi.

Akiwa amepoteza jezi yake namba 19 kwa Lamine Yamal, hajapewa jezi nyingine na hivyo hana nafasi kwenye kikosi cha kwanza.

AS imeripoti Barca "haikufikiria" kumsajili Roque kwa LaLiga.

Lakini Pau Cubarsi, Pablo Torre, Pau Victor na Marc Casado wote wamepandishwa kwenye kikosi cha wakubwa, kila mmoja akipewa namba za jezi kati ya moja na 25, kwa mujibu wa sheria za LaLiga.

Ansu Fati pia amehifadhi nafasi yake, licha ya kutoichezea klabu hiyo kwa mwaka mmoja na tena kusumbuliwa na majeraha wakati wa mkopo ambao haukufanikiwa katika Klabu ya Brighton & Hove Albion.

Eric Garcia pia amerejea kwenye kikosi tangu alipocheza kwa mkopo kwa majirani zao Girona msimu uliopita.

Dani Olmo bado hajasajiliwa LaLiga, lakini Barcelona wanaaminika kufanyia kazi fedha



ili kutoa nafasi kwa mshindi huyo wa Euro 2024, ambaye tayari amekabidhiwa jezi namba 20.

Hata kama kulikuwa na mtaji wa kumsajili Roque, hakuna namba za jezi za kikosi cha kwanza.

Jezi hiyo ya 25 bado ni ya bure lakini imetengwa kwa makipa pekee katika soka la Hispania.

# NBC KUJA KIVINGINE BAADA YA TUZO WACHEZAJI BORA KILA MECHI

**Na Mwandishi Wetu**

MDHAMINI Mkuu wa Ligi Kuu ya NBC, Benki ya NBC, imesema mpango mpya wa utoaji wa tuzo kwa wachezaji bora wa kila mechi za ligi hiyo ni mwendelezo tu wa jitihada zao katika kunogesha ligi huku ikibainisha kuwa bado kuna mipango mizuri zaidi inaandaliwa ikilenga kuongeza mvuto, ushindani na vinwango kwenye ligi hiyo.

Kauli ya mdhamini huyo anaedhamini ligi tatu muhimu za mpira wa miguu hapa nchini, imekuja huku tayari ikishuhudiwa wachezaji kutoka klabu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu ya NBC, wakipatiwa tuzo za uchezaji bora kwenye mechi nne ambazo zimekwishachezwa kwenye mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo.

Mlinda mlango wa timu ya Pamba Jiji FC ya jijini Mwanza, Yona Amosi Abel, ndiye aliyefungua pazia la kutwaa tuzo hizo baada ya kuibuka mchezaji bora kwenye mechi ya kufungua pazia la ligi hiyo baina ya timu hiyo na Prisons ya mkoani Mbeya, mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza na kumalizika kwa suluhu.

Maofisa wa NBC Tawi la Mwanza wakiongozwa na Meneja wa Benki hiyo tawi la Nyanza jijini humo, Innocent Ngavatula, ndio pia waliofungua pazia la kukabidhi zawadi hizo wakifuatiwa na maofisa wengine wa benki hiyo katika mikoa tofauti zilipochezwa mechi za ligi hiyo ikiwamo Kigoma, Mbeya na Dar es Salaam.

"Tukiwa tumetambulisha rasmi tuzo hizi kwenye kila mechi ya ligi hii, tayari tumekabidhi jumla ya tuzo nne kwa wachezaji wa klabu tofauti ambazo tayari zimecheza michezo yao. Mbali na Yona Amosi wa Pamba jiji tuzo hizi pia tumekabidhi kwa mlinzi wa kati wa Klabu ya Mashujaa, Ibrahim Ame, Kiungo Emmanuel Keyekeh 'The Sniper' kutoka Singida Black Stars na Beki wa Simba SC, Che Fondoh Malone," alitaja David Raymond, Mkuu wa Idara ya Masoko benki hiyo.

Kwa mujibu wa Raymond, ujio wa tuzo hizo za wachezaji bora kila mechi haujaathiri kwa namna yoyote utaratibu wa awali wa kutoa tuzo za mchezaji na kocha bora wa ligi hiyo kila mwezi.

"Lengo haswa ni kuhakikisha ndani ya muda mfupi tunakuwa na vionjo vingi zaidi kwenye ligi hii tukilenga kuongeza chachu na ushindani kwenye ligi husika kupitia utambuzi wa jitihada zinazofanywa na wachezaji wetu na mabenchi yao ya ufundi katika ubora."

"Kupitia ushirikiano wetu na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), pamoja na wadau wengine wakiwAmo wataalam mbalimbali wa mchezo huu, tutaendelea kubuni mambo mazuri yenye tija zaidi kwa faida ya wadau wote wa ligi hii wakiwamo pia mashabiki," alibainisha.

Ikiwa kama mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu ya NBC, Ligi ya Championship na Ligi ya Vijana, benki ya NBC imekuwa ikitoa huduma mbalimbali za kibenki zinazolenga kuzisaidia klabu zinazoshiriki ligi hiyo ikiwamo utoaji wa mikopo ya mabasi kwa baadhi ya klabu na bima za afya kwa wachezaji na mabenchi ya ufundi.

"Zaidi tumekuwa tukishiriki katika kuandaa sherehe za ubingwa kwa washindi wa ligi zote tunazozidhamini pamoja na kudhamini matukio mbalimbali ya kimichezo yanayoandaliwa na TFF na wadau wengine wa michezo hapa nchini ikiwamo serikali," alisema.

# Tabora Utd kumalizia hasira kwa Namungo

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Tabora United, imesema baada ya kufungwa mabao 3-0 dhidi ya Simba Jumapili iliyopita, Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam, sasa hasira zao wanazielekeza kwa Namungo katika mechi inayofuata.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala, alisema wamekubali kuwa wamepoteza mechi kihalali dhidi ya Simba kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ugeni wa wachezaji wengi kwenye kikosi, lakini mchezo huo umewapa mazoezi tosha ya kujua uzito wa mechi za Ligi Kuu.

"Tumekubali tumefungwa, lakini tumefunga na timu kubwa ya Simba, kwa hiyo nadhani mechi inayofuata tutapata ushindi kwa sababu hatuchezi tena na mnyama, bali Namungo.

"Mechi iliyopita imetupa mwelekeo na mazoezi tosha ya kujua uzito wa mzani wa Ligi Kuu, nadhani sasa wachezaji watakuwa wanaelewa nini wanatakiwa kufanya baada ya mchezo huo," alisema.

Mwagala alisema sababu kubwa ya kupoteza mechi hiyo ilikuwa ya kwanza, halafu inacheza na timu kubwa, huku ikiwa na wachezaji wengi wapya.

"Tumesajili wachezaji 28 msimu huu, lakini kati ya hao, ni sita tu waliokuwa msimu uliopita, kwa hiyo utaona kuwa 22 wote ni wapya, unakwenda kucheza na timu kama Simba, labda kama tungecheza na timu nyingine, hilo tumemaliza nadhani mechi inayofuata tutawaonesha mashabiki wa soka kuwa Tabora United si timu ya mchezo kama wanavyofikiria," alisema. Alisema Kocha Mkuu, Mkenya, Francis Kimanzi, ameendelea na mazoezi ya kukiunganisha kikosi hicho ambacho kilionekana kukosa muunganiko katika mchezo dhidi ya Simba.

Tabora United ipo jijini Dar es Salaam, ikijiandaa na safari ya kwenda mkoani Lindi kucheza mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo, Jumapili ijayo, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa.




Mkuu wa Kitengo cha Biashara Benki ya NBC, Ibrahimu Nzutu (Kulia), akikabidhi tuzo kwa Beki wa timu ya Simba, Che Fondoh Malone, aliyetangazwa mchezaji bora kwenye mechi ya Ligi Kuu ya NBC mzunguko wa kwanza dhidi ya Tabora United iliyopigwa mwishoni mwa wiki katika Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam. Katika mechi hiyo Simba iliibuka na ushindi wa mabao 3-0. Benki ya NBC ni mdhamini mkuu wa ligi hiyo. **MPIGAPICHA WETU**

# Ateba kamili Simba SC kuivaa Fountain Gate

INATOKA UK. 24

"Tumeachana na Freddy baada ya mwalimu Fadlu kutoridhishwa na kiwango chake na kutaka apatiwe mshambuliaji mwingine, na nafasi yake ndiyo imechukuliwa na Ateba.

"Tumemuuza klabu gani, sitaki kuisemea, klabu yake ndiyo ina mamlaka ya kumtangaza, unajua siku hizi taarifa zinauzwa, waliomnunua ndiyo wana mamlaka ya kumtangaza," alisema Ahmed.

Freddy sasa ataungana na wachezaji wenzake wa zamani wa Simba waliocheza pamoja msimu uliopita, viungo Babacar Sarr na Sadio Kanoute na watakuwa chini ya aliyekuwa Kocha Mkuu wa ,Wekundu wa Msimbazi' hao, Abdelhak Benchikha.

Wakati huo huo, Ahmed alisema kwa mujibu wa daktari wa timu hiyo, amebainisha kuwa jeraha alilopata mshambuliaji Joshua Mutale, Jumapili iliyopita dhidi ya Tabora United, si kubwa na tayari ameanza matibabu.

Alisema kikosi hicho kimerejea mazoezi baada ya mechi iliyopita, huku kocha akirekebisha mapungufu yaliyojitokeza katika mchezo huo.

"Ukweli tumeshinda, lakini ukiiangalia kwa jicho la kitaalamu, utaiona kuna mapungufu kidogo, ukiangalia nafasi hazikutengenezwa nyingi, na zilizotengenezwa hazikutumika sawasawa, kwa hiyo mwalimu bado ana kazi ya kukisuka upya kikosi chetu.

"Kina wachezaji wengi wapya, lakini wanaonekana wana uwezo mkubwa kwa kucheza kwa kasi, kukimbia, kukaba na kufanya mambo mengi kwa usahihi tofauti na kike cha msimu uliopita, lakini hakijakuwa na muunganiko unaotakiwa na wachezaji kuzoeana uchezaji wao, wakishazoeana itakuwa balaa kubwa," alisema.

Simba kwa sasa ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu baada ya mchezo mmoja tu dhidi ya Tabora United ambao ilishinda mabao 3-0, mechi ikipigwa Uwanja wa KMC uliopo Mwenge, Dar es Salaam.

Mchezo unaofuata, Simba inatarajiwa kucheza na Fountain Gates kwenye uwanja huo, Jumapili wiki hii.

# Gamondi ampa 'mchongo' Dube, Fifa yawashukia

INATOKA UK. 24

"Bado hatujamaliza, tunamchezo wa pili nao ni muhimu, nataka kuona tunacheza vizuri zaidi na kupata ushindi mkubwa, tunaweza kufanya hivyo," alisema Gamondi.

Yanga itaumana na Vital'O Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kumalizia kazi waliyoianza wiki iliyopita ya kusaka tiketi ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Michezo

Jumatano Agosti 21, 2024

Nipashe

## Napoli yapambana kumbakiza Osimhen

UKURASA 21






Mshambuliaji wa Yanga, Prince Dube, akishangilia bao lake dhidi ya Vital'O kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Azam Compelx , Dar es Salaam Jumamosi iliyopita na timu yake kushinda mabao 4-0. **MPIGAPICHA WETU**

# Ateba kamili Simba SC kuivaa Fountain Gate

## ●●● Ni wakati Benchikha akimvuta Freddy USM Alger kuungana na Kanoute, Babacar Sarr ambao...

**Adam Fungamwango na Faustine Feliciane**

KLABU ya Simba imesema straika wake mpya, Lionel Christian Ateba, amekamilisha taratibu zote za kisheria zilizomkwamisha kucheza mechi iliyopita, hivyo anatarajiwa kuonekana katika mchezo wa Jumapili ijayo dhidi ya Fountain Gate, utakaochezwa, Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema straika wao mpya, Ateba, hakuonekana katika mechi ya Jumapili iliyopita dhidi ya Tabora United kutokana na kutokamilisha baadhi ya taratibu ambazo zingemruhusu kucheza.

"Alikuwa yupo fiti kucheza kwa sababu alikuwa kwenye ,pre season' na timu yake ya USM Alger ya Algeria, lakini hakuwa amekamilisha taratibu ambazo zingeweza kumruhusu kucheza, unajua ilikuwa ni mwisho wa wiki, siku za mapumziko, kulihitajika baadhi ya mambo ya kisheria yakamilike, lakini ninavyokwambia kwa sasa kila kitu kiko tayari.

"Ameshapata kibali cha kuishi nchini, cha kufanya kazi, leseni, pamoja na Uhamisho wa Kimataifa (ITC), kwa maana hiyo sasa ataanza kuonekana tutakapocheza na Fountain Gate, kama ataanza au ataingia kipindi cha pili, hiyo ni kazi ya mwalimu, lakini kila kitu kiko tayari, Ateba ataonekana siku hiyo," alitamba Ahmed.

Meneja Habari huyo pia, amethibitisha klabu hiyo, kumpiga bei straika wao, Freddy Michael ambaye ilimsajili katikati ya msimu uliopita kutoka Klabu ya Green Eagles ya Zambia, huku taarifa zikieleza ametimkia USM Alger, timu ambayo ametoka Ateba.

INAENDELEA UK. 23

## Gamondi ampa 'mchongo' Dube, Fifa yawashukia

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, akisema mshambuliaji wake, Prince Dube, anahitaji kuongeza umakini kidogo mbele ya lango la wapinzani ili kuweza kufunga mabao mengi, Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), limeita klabu hiyo kuilipa Bechem United FC ya Ghana Dola 80,000 sawa na Sh. milioni 216.9 za Tanzania.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Yanga kushindwa kesi iliyofunguliwa na Klabu ya Bechem FIFA, hicho ikiwa ni gharama ya ada ya uhamisho ya mchezaji Augustine Okrah waliyemsajili Januari mwaka jana.

Kwa mujibu wa barua ya FIFA kwenda Yanga iliyosambaa jana katika mitandao ya kijamii, klabu hiyo inatakiwa kuwalipa Waghana hao ndani ya siku 45 baada ya hukumu hiyo iliyotolewa jana.

Jitihada za kuwapata viongozi wa Yanga kuzungumzia maamuzi hayo ya FIFA hazikufanikiwa kwa kuwa simu za mkononi za viongozi hao ziliita bila majibu.

Kuhusu Gamondi na Dude, kocha huyo amesema ni mshambuliaji mzuri na mwenye uwezo mkubwa, lakini kuna baadhi ya mambo yanamfanya ashindwe kufunga mabao mengi.

Alisema tayari amekaa naye na kumpa maelekezo na kama atayafuata atakuwa miongoni mwa washambuliaji watakaokuwa wakifunga mabao mara kwa mara.

"Nataka muda mwingi tukiwa tunashambulia awe ndani ya eneo la hatari la wapinzani, tunatengeneza nafasi nyingi, lakini mara nyingi anakuwa hayupo eneo husika,

"Naamini akifanya hivyo na kuongeza umakini atakuwa akitufungia magoli mengi, ni mshambuliaji mzuri, ana nguvu na ufundi mwingi," alisema Gamondi.

Aidha, alisema kwa sasa anaendelea kuwapa maelekezo wachezaji wake kuelekea kwenye mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya awali dhidi ya Vital'O.

Kuhusu mchezo huo, Gamondi, alisema licha ya ushindi mnono walioupata kwenye mchezo wa kwanza wa mabao 4-0 katika Uwanja wa Azam Complex, hawatawadharau wapinzani wao hao.

INAENDELEA UK. 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042